SportPesa
TZS. 846,297,200
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**ASKARI** wa JWTZ matatani tuhuma kumuua baba yake

UKURASA 16


BUFE
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Nipashe
SHULE J3; HITAJI SH. 980,000; KAPATA SH. 45,000...
Walezi bibi & babu hawana hata senti, binti kafaulu 'A', shule vipaji maalum
• Baba kawatelekeza, mama katoweka, wadogo zake 2

UKURASA 11

Nipashe
Ijumaa Januari 14, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580825
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/th
MWA... JAMII

# RAIS SAMIA ATEMA NYONGO

**ATAKA** taasisi urais iheshimiwe, aonya upendeleo, undugu ajira, aagiza... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan.



UKURASA 2

Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe (katikati) na wenzake wakiwa kwenye chumba cha Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, mkoani Dar es Salaam jana katika kesi inayowakabili. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mwanasheria wa Airtel aeleza alivyochunguza simu ya Mbowe

## Polisi watatu wajeruhiwa wakimkamata mtuhumiwa wa ujambazi

UKURASA 3

UKURASA WA 4

## MWINYI APONGEZA USHIRIKIANO JKT, JKU



RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amepongeza ushirikiano uliopo kati ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi...

UKURASA WA 4

## PROF. MKENDA AGEUKIA MITAALA ELIMU

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema anatarajia kutafuta wataalamu wabobezi katika ...

UKURASA WA 4

## AFUNGWA MIAKA MIWILI KUJIFANYA OFISA TRA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Dodoma, imemhukumu mkazi wa Dar es Salaam, Kitareti...

**MICHEZO** CONTE AJITETEA KUMWACHA BENCHI LLORIS UK.22

**MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akimwapisha Said Shaibu Mussa kuwa Balozi wa Tanzania nchini Kuwait, Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma jana. PICHA: IKULU

# Rais Samia atema nyongo

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewapa kibarua mawaziri na naibu mawaziri akiwataka kuangalia upya sera na sheria huku akikemea utoaji ajira kwa undugu na urafiki pamoja na kuwaonya watumishi wasiowajibika.

Alisema hayo jana katika kikao maalumu cha mawaziri na naibu mamaziri aliowateua hivi karibuni na wale waliokuwapo kabla ambao wanaendelea, jijini Dodoma na kuwataka kuwa wabunifu.

Alisema ni muhimu viongozi hao wakaangalia , namna ya kuboresha sheria, sera na taratibu za uendeshaji wa wizara na taasisi zao, ili kuhakikisha zinafanya kazi kuleta matokeo mazuri zaidi kwa wananchi.

"Ajira za undugu na urafiki ni miongoni mwa vitu vinavyoharibu taasisi za serikali. Unapoajiri ndugu, rafiki zako ndani ya taasisi kwa sababu mmekua pamoja, ni rafiki zako, mnaua taasisi. Naomba sana mkayazingatie haya.

"Ni bora kutengeneza timu yako ya kazi ambayo unajua kwamba mtachapa kazi na si tu eti kwa sababu ni rafiki au ndugu zako," alisema.

Pia alisema kwa watumishi wasiowajibika, ni vyema wakajitafakari kulingana na viapo vyao.

"Dunia nzima, nchi inayoitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni moja tu na wananchi walioko humo ni sisi. Kwa hiyo kama ni kuibomoa ni sisi tutaibomoa, kama ni kuijenga ni sisi, kama kuipa sifa duniani ni sisi.

"Sisi tuliobahatika kuwa katika nafasi mbalimbali, wizarani, mashirika na taasisi zote za serikali yetu ambazo sheria na miongozo yetu imekubali ziwapo, tuna wajibu mkubwa na tumebeba hiyo nchi na watu wake," alisema na kuwataka kuacha ubinafsi na badala yake kufanya kazi kuwaletea maendeleo wananchi.

"Lakini ukijitizama wewe zaidi kuliko wajibu wako uliopewa, hutakuwa unafanya vyema, kila mmoja wetu akajipime anafanya nini. Je, anawajibika? Je kile kiapo anakitekeleza? na kama unakwenda kinyume cha kiapo ulichokiapa kwa dini yako, nenda kajitathmini.

Hakuna atakayeweza kupasua mioyo yenu akaingia vifuani mwenu akajua huyu anafikiria nini, huyu ni mkweli, huyu si mkweli. Kila mtu anajijua, lakini ujue kwamba umebeba jukumu zito na umebeba wananchi wote wanaotaka kwende kuhudumiwa," alisisitiza.

Pia alisema kila mmoja katika taasisi yake anatakiwa kuwa mbunifu, afanye kazi kwenye wizara yake na kuichukulia kama ni yake binafsi, angependa iendeshweje, ifanye nini ili faida ionekane na hatimaye wananchi wajisikie kuwa wanahudumiwa na kwamba mawaziri na naibu mawaziri watambue kwamba wao ndio wenye timu yote.

**TAASISI YA URAIS**

Rais Samia aliwataka wateule hao pamoja na viongozi anaowachagua, kuheshimu taasisi ya urais anayoiongoza hata kama wanamchukia huku akibainisha kuwa nafasi ya urais ni taasisi na si mtu, hivyo kinachotakiwa kuheshimiwa ni taasisi.

"Urais ni taasisi na si mtu. Mtu inakuwa tu tukifuata Katiba yetu na mambo mengine na kati yetu mmoja wetu lazima awe Rais, akae pale kuangalia mambo yanavyokwenda.

"Urais ni taasisi ambayo inakuja na mamlaka yake, inakuja inatoa miongozo. Kwa yeyote anayekuwapo pale anafanyia kazi taasisi ya urais. Sasa kama humpendi aliyepo, penda nchi yako," alisema na kuwataka kutambua kuwa mamlaka ya uongozi wowote inatoka kwa Mungu.

"Kama unaona Samia aliyepo simpendi tu, usimpende yeye ukapuuza na yote yanayozunguka hiyo taasisi. Yale yanayotokana na taasisi anayoiongoza, yaheshimu, mchukie yeye tu," alisisitiza.

Rais aliwakumbusha wateule hao kuwa kiapo ambacho viongozi hao wamekiapa ni kikubwa na kwamba ni vema wakakiheshimu.

**SHAURIANENI**

Rais Samia aliwataka viongozi hao kushauriana na kuonyana kwa hekima wanapoona kuna mambo yanaharibika badala ya kutumia ubabe.

"Hivi mnaijua muhali? "Ni hali ambayo labda namwona Waziri Mkuu wangu ana tatizo lakini unamtizama usoni humwambii, mwisho wa siku linakuja kuharibu kazi. Sasa kule kutokutaka kuambizana, kutokutaka kuchukuliana hatua, kutokutaka kuonyesha kumkera mtu kwa kumwambia kasoro yake hiyo ndiyo muhali.

"Kwa hiyo mnakokwenda huko, kama mwenzio ana tatizo, itaneni kistaarabu, si kutukanana. Unamwambia unajua ndugu yangu katika kazi zako nimeona moja, mbili, tatu. Tungepita njia hii tungekwenda vizuri zaidi kuliko huku, siyo ile kikomandanti, njoo hapa, halafu unamwambia. Hatuwezi kwenda hivyo, nitakwenda kumwambia mama mimi, aaahaa, rekebishaneni kwanza huko ndani.

"Ujue kama wewe unaitwa Waziri, ni mkubwa wa wengine chini, hata kama amekuzidi umri, lako wewe ni hekima, busara, jinsi ya kudili na wenzio, kuliko ubabe, kutunishiana misuli. Mkianza kutunishiana misuli na kutishiana ndiyo matatizo yanaanza ndani ya taasisi, ndani ya sekta zenu, kwa hiyo kuondosheana muhali kama kuna tatizo lisemwe ili twende mbele."

Rais Samia alisema wakianza kutunushiana misuli na kuonyeshana ubabe kutaharibu taasisi na kuumiza wananchi.

**MPANGO AWAPA SOMO**

Naye Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, aliwataka mawaziri hao kujiepusha kujihusisha na kashfa wakati wa utendaji kazi wao ikiwamo rushwa na ubadhirifu, ulevi na uchawi.

Akihitimisha mkutano maalumu wa mawaziri hao, Dk, Mpango alisema: "Si vyema Waziri au Naibu Waziri kutuhumiwa na mambo ya ovyo yakiwamo ya rushwa hasa ya ngono, ulevi na uchawi. Hivyo haviendani na maadili ya uongozi na kufanya hivyo kunakuondolea hadhi yako."

"Kila mmoja azingatie maadili na miiko ya kazi yake. Tushirikiane katika mgawanyo wa kazi zetu, ikiwamo kuwahudumia wananchi. Kwa mfano anakuja mzee kudai pensheni halafu unamwambia rudi tu faili lako silioni... je, angekuwa baba au mama yako amekuja na shida ya namna hiyo ungemjibu hivyo? Tuguswe na shida za wananchi."

Dk. Mpango pia alikemea vitendo vya viongozi hao kunyanysa watumishi walio chini yao.

"Tulikuwa na kesi ya ovyo. Kiongozi anaondoka kurudi Dar es Salaam, anafika kununua nyanya na vitunguu na dereva wake akashuka kununua akaviweka kwenye gari. Kiongozi huyo alimwambia shusha. Sasa kiongozi wa namna hiyo, hata utu hakuna kwa sababu tu yeye ni dereva au ni mhudumu," alisema.

# Shahidi aeleza alivyochunguza miamala katika simu ya Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI wa tisa wa Jamhuri, Gladis Fimbari (36) katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, na wenzake watatu, amedai alipewa jukumu la kuchunguza miamala na usajili wa namba tatu za simu.

Fimbari ambaye ni Mwanasheria wa kampuni ya simu za mkononi ya Airtel, amedai kuwa miongoni mwa simu hizo ni pamoja na inayodaiwa kuwa ya Mbowe, Simu nyingine ni ya Luteni Dennis Urio.

Alidai hayo jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joachim Tiganga wakati akitoa ushahidi kwa kuongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando.

Alidai kuwa Julai 2, 020 akiwa ofisini Morocco, Dar es Salaam, Mkuu wake wa idara alimpa kazi ya kushughulikia miamala ya fedha ya namba tatu.

Shahidi alitaja namba hizo kuwa ni 0782 237913 ambayo katika usajili alidai ilikuwa inamilikiwa na mshtakiwa Halfani Bwire, ya pili 0787 555200 usajili ukionyesha ni ya Luteni Urio na 0784 779944 ambayo katika usajili ilikuwa inamilikiwa na Mbowe.

Katika uchunguzi huo, alidai kuwa alitumia mifumo miwili, wa kwanza wa kupata taarifa za miamala unaoitwa MOBIQUIT unaochukua taarifa na kuhifadhi. Mfumo wa pili alidai unaitwa AGILE, ambao unatumika kupata taarifa za usajili za mteja na katika kazi hizo anatumia kompyuta mpakato au ya kawaida.

Mwanasheria huyo alidai vitendea kazi vimeunganishwa na mifumo ya Airtel na haiwezekani kufanya jambo lolote na pia vimeunganishwa na mfumo wa kutoa taarifa pale inapofanyika kinyume.

Alidai kuwa alipoanza kuchunguza, aliingia kwenye mfumo na kuingiza namba moja ya simu iliyoombwa taarifa yake kisha ikatoa taarifa ambayo aliihakiki kujiridhisha kisha akaichapisha. Alidai kuwa alifanya hivyo kwa namba zote tatu.

Alipohojiwa kama nyaraka alizoandaa akiziona atazikumbuka, alidai atazikumbuka kwa sababu kuna jina lake, saini yake na muhuri wa Airtel.

Fimbari alidai kuwa katika nyaraka hizo aliambatanisha na barua ya maombi kutoka ofisi ya uchunguzi ya Julai Mosi, 2021 iliyoonesha jalada CD/IR/2097/2020 ikiwa na namba tatu zilizoombewa taarifa.

Shahidi aliomba kutoa taarifa hizo kama kielelezo na mawakili wa utetezi, wakiongozwa na Peter Kibatala hawakuwa na pingamizi. Mahakama ilipokea na kuvipa namba vielelezo hivyo.

Katika uchunguzi wake, alidai kuwa Julai 20, 2020 namba 0784 779944 ilifanya muamala kwenda kwenye namba 0787 555200 wa Sh 500,000, muamala wa pili Sh. 199,000 na wa tatu ulifanyika Julai 31, 2020 kutoka namba 0784 779944 kwenda namba 0782 237913 ya Halfani Bwire wa Sh. 80,000.

Luteni Urio ni Mwanajeshi anayedaiwa katika kesi hiyo alitumwa na Mbowe amtafutie makomandoo waliostaafu au waliofukuzwa kazi ili wafanye vitendo vya kigaidi huku maelezo ya onyo ya washtakiwa yakidai kwamba Urio aliwatafutia kazi ya kumlinda Mbowe washtakiwa watatu katika kesi hiyo.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Bwire, Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya ambao wanashtakiwa kwa kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei na Agosti, 2020.

## HABARI KITAIFA

# Mtuhumiwa ujambazi ajeruhi polisi wakimkamata

**Na Francis Godwin, IRINGA**

ASKARI polisi watatu mkoani Iringa, wamejeruhiwa sehemu mbalimbali za miili yao wakati wakimkamata mtuhumiwa sugu wa makosa ya wizi wa pikipiki na uvunjaji, Godson Kahemela.

> **"Mtuhumiwa huyu wakati anakamatwa aliwajeruhi askari watatu sehemu mbalimbali na alipokamatwa alikutwa na panga aliloliandika KIFO, akimaanisha kuwa yuko tayari kufanya mauaji kama ambavyo alitaka kuwafanyia askari wakati anakamatwa," alisema Kamanda Bukumbi.**

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Allan Bukumbi, alisema askari hao walijeruhiwa wakati wakimdhibiti mtuhumiwa huyo ambaye amekuwa akijihusisha na matukio ya uvunjaji katika maeneo mbalimbali Manispaa ya Iringa.

Kamanda Bukumbi alisema mtuhumiwa huyo wakati anakamatwa alikutwa na panga.

"Mtuhumiwa huyu wakati anakamatwa aliwajeruhi askari watatu sehemu mbalimbali na alipokamatwa alikutwa na panga aliloliandika KIFO, akimaanisha kuwa yuko tayari kufanya mauaji kama ambavyo alitaka kuwafanyia askari wakati anakamatwa," alisema Kamanda Bukumbi.

Wakati huo huo, Kamanda Bukumbi alisema Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na maofisa uhamiaji wa mkoa wa Iringa wamewakamata wahamiaji haramu 40, raia wa Ethiopia, ambao wanadaiwa kutelekezwa kwenye lori baada ya kuingia nchini kinyume cha utaratibu.

Alisema wahamiaji hao walikamatwa Wilaya ya Iringa katika Barabara Kuu ya Iringa - Mbeya baada ya kutelekezwa katika lori aina ya Mitsubishi Fuso lenye namba za usajili T 517 DJY mali ya Deogratius Kimambo, mkazi wa mkoani Kilimanjaro.

Kamanda Bukumbi alisema kukamatwa kwa wahamiaji hao ni mwendelezo wa operesheni mbalimbali zinazoendelea mkoani Iringa zenye lengo la kupambana na matukio ya uhalifu.

Alisema baada ya kufanya upekuzi katika gari hilo walikutwa wahamiaji hao wakiwa wameingia nchini kupitia mpaka wa Namanga, wakisafirishwa kwenda mpaka wa Tunduma.

Pia alisema Januari 11, mwaka huu, polisi kwa kushirikiana na maofisa wa Hifadhi ya Taifa Ruaha, waliwakamata watu wawili wakisafirisha meno ya tembo vipande 19 pamoja na jino moja la kiboko kwa kutumia pikipiki.

Kamanda Bukumbi aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Ezekiel Patrick (43) na George Ng'umbi (25). Kadhalika, alisema Januari 7, mwaka huu, maeneo ya Kitongoji cha Magunga Bondeni, Kiponzero wilayani Iringa, askari polisi walimkamata Paul Kalinga (47) akiwa na meno mawili ya tembo.

# Mamia wamuaga Ngapemba Dar

**Na Salome Mwasamale**

MAMIA ya wanahabari, ndugu, jamaa na marafiki, jana walijitokeza kuaga mwili wa aliyekuwa Ofisa Habari wa Mkoa wa Mwanza, Abeli Ngapemba (53) (pichani), aliyefariki dunia kwenye ajali ya gari Busega, mkoani Simiyu.

Waombolezaji hao walijitokeza kuifariji familia ya Ngapemba pamoja na kushiriki ibada ya kuaga mwili wake iliyofanyika katika Kanisa Katoliki Bikira Maria wa Mlima Kalmel, Bunju A, Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa ibada hiyo, Askofu Msaidizi kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Henry Mchamungu, aliwataka waombolezaji kutumia kifo cha Ngapemba kama njia sahihi ya kumtumikia Mungu kwa kuwa Biblia inawataka kuwa tayari wakati wote kwa kuwa hawajui siku wala saa ya kutwaliwa na Mungu.

"Sisi binadamu tunapofariki hatujui tunaenda wapi ndiyo maana tunawaombea waliotutangulia ili Mungu apate kuwasamehe makosa yao na kuwakaribisha katika ufalme wa Mungu. Wanaoamini katika ufufuo wa wafu, kwa wanao amini kifo hakitishi kwa kuwa ndiyo mwanzo wa maisha mengine ila kwa wasioamini kifo kinatisha tena marehemu wanaonekana wameenda kwenye maangamizi," alisema.

Alisema kifo kinahitimisha maisha ya duniani na kinaanzisha maisha mapya ya mbinguni, lakini hakipigi hodi kinakuja muda wowote hivyo aliwataka waombolezaji kukesha wakimwomba Mungu kwa kuwa hawajui siku wala saa ya kutwaliwa kwao kama ilivyokuwa kwa Ngapemba.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Kaimu Katibu Trawler Mkoa huo, Tutuba Mangazini, alisema ujio wa Ngapemba katika mkoa ulileta mabadiliko makubwa ya kiutendaji, hivyo atakumbukwa daima kwa uchapa kazi wake.



Naye, Mdogo wa Marehemu, Padri Titus Ngapemba, alisema katika enzi za uhai wake, walishuhudia maisha yenye ushuhuda mzuri, lakini alimshukuru Mungu kwa kuwa alizungumza na kaka yake saa mbili kabla ya ajali.

Alisema wamepokea salamu nyingi za pole kutoka kwa ndugu, jamaa na marafiki. Alisema Ngapemba alikuwa mtu wa 'network' (mtandao), hivyo wamezipokea kama familia.

Mwili wa Ngapemba uliwasili nyumbani kwake Bunju juzi usiku ukitokea mkoani Mwanza baada ya kumalizika kwa ibada ya pamoja iliyofanyika katika viwanja vya Nyamagana na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel.

Ngapemba alifariki dunia Januari 11, mwaka huu, majira ya saa 12:45 asubuhi katika ajali ya magari mawili, lililokuwa limebeba waandishi kwenda Ukerewe na Toyota Hiace iliyokuwa ikienda Mwanza ambayo yaligongana uso kwa uso na kusababisha vifo vya watu 14 na sita kujeruhiwa.

Ngapemba ameacha mjane na watoto watatu. Bwana alitoa na Bwana ametwaa, jina lake lihimidiwe. **Amina.**


Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Sky Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O.Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania

Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA WA WATANZANIA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | AINA NA SEHEMU YA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | PATRIC MARTIN MLWILO | NYUMBA | LESENI YA MAKAZI – KIGOGO MBUYUNI | JOFORTE AUCTION MART | 28-01-2022 |
| 2 | SADA ABDALLAH LAISER | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - TEGETA | TULVIN INVESTMENT | 28-01-2022 |
| 3 | VERONICA IMBYANDUMI KIMARO | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - KIGOGO | DIAMOND - RECOVERIES | 28-01-2022 |
| 4 | DICKSON MKOSA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO- CHALISUKA MADIBIRA | PAMOJA AUCTION MART | 28-01-2022 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika ofisi za wakuu wa wilaya wanaohusika.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

166500



Leonard Cheshire | Tanzania Cheshire Foundation

## SEEKING PASSIONATE AND ETHICALLY MOTIVATED TANZANIAN PROFESSIONALS.

**Tanzania Cheshire Foundation (TCF) in partnership with Leonard Cheshire (LC) have been awarded a three-year grant to deliver an innovative Inclusive-Education Project in Tanzania.**

Tanzania Cheshire Foundation (TCF) in partnership with Leonard Cheshire (LC) have been awarded a three-year grant to deliver an innovative Inclusive-Education Project in Tanzania.

TCF and LC in partnership, are excited to be commencing work as part of a wider consortium on this new multi-year Disability Inclusive Development (DID) project in Shinyanga City, Shinyanga district council in Shinyanga region and Misungwi in Mwanza region of Tanzania, in line with the National Inclusive Education Strategy (NIES). The project aims to increase the enrolment and retention of children with disabilities in education, to increase their learning and improve their life-chances focusing on inclusive education for pre-primary and primary school-going age children.

LC is part of the Inclusive Futures consortium, funded by the Foreign, Commonwealth and Development Office (FCDO). The 16 Inclusive Futures partners are working together to include people with disabilities in health, work, education, and tackle stigma and discrimination through the Disability Inclusive Development (DID) programme. Together we are using a range of innovations to promote the importance of disability inclusion, aligning closely with the work of governments.

TCF and LC in partnership as part of a wider consortium will work closely together with government officials and OPDs as well as a range of stakeholders at local level, striving to improve the implementation and accountability of inclusive education in Tanzania.

**We are looking for experienced disability inclusion role models, and ethically motivated Tanzanian professionals for three critical positions, available to start immediately**

**Consortium Project Manager** *(45,000,000 – 52,000,000 TZS)*
to coordinate delivery on behalf of the Consortium project
https://careers.leonardcheshire.org/jobs/vacancy/consortium-project-manager--08823-tanzania/8843/description/

**National Technical Advisor (IE)** (part-time 3 days p/week c.28,800,000 – 34,800,000 TZS pro-rata)
to provide guidance and technical advice on Inclusive Education
https://careers.leonardcheshire.org/jobs/vacancy/national-technical-adviser--08825-tanzania/8845/description/

**Monitoring Evaluation and Learning Manager (MEL)** *(38,000,000 – 43,000,000 TZS)*
to lead on MEL and accountability practices
https://careers.leonardcheshire.org/jobs/vacancy/monitoring-evaluation--learning-manager-08824-tanzania/8844/description/

**About you –** First and foremost, you must be passionate about and committed to disability inclusion and safeguarding and be personally driven to make a difference in the lives of children. You must have proven experience of working in a consortium programme dealing effectively with multiple stakeholders across government, OPDs, and with local community groups. This is a real opportunity to make a meaningful impact in Tanzania.

**Application process -** All interested candidates must apply via the links associated to the vacancies. Only candidates who apply online will be considered. In your application, please include your CV and a cover letter giving your motivation to apply and your availability). Full job description details are available in each link. We welcome applications from all sections of the community and actively encourage professionals with disabilities to apply. This will be a fast-faced recruitment process and we are seeking for candidates available to start immediately.

*We reserve the right to close this vacancy once suitable candidates have been identified.*

166507

# Prof. Mkenda ageukia mitaala elimu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema anatarajia kutafuta wataalamu wabobezi katika elimu wakiwamo wastaafu ili kupata mchango wao wa kuboresha elimu ikiwamo uboreshaji wa mitaala.

Prof. Mkenda amesema katika kufanya hivyo, atatenga wiki tatu kuzungumza na watumishi wa wizara na kupitia nyaraka muhimu ili kufanya uchambuzi ili kuboresha elimu na kuleta tija kwa maendeleo ya taifa.

Aliyabainisha hayo jana, jijini hapa wakati wa makabidhiano ya ofisi kutoka kwa mtangulizi wake, Prof. Joyce Ndalichako.

Mkenda alisema wizara hiyo ni nyeti, hivyo inatakiwa kutendewa haki kwa kufanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na watumishi.

"Wizara hii si ya kuchezea ni wizara nyeti sana. Ukiichezea inahitaji si kubadilisha badilisha mambo, tutalichanganya taifa," alisema.

"Pia ili kufanya kazi vizuri, naomba ushirikiano na msiwe na nidhamu ya uoga pale mnapoona kuwa mambo siyo msisite kuniambia ukweli kwani nyie ni wazoefu wa wizara hii muhimu," alisisitiza.

Aliwataka watumishi kutokuwa na nidhamu ya uoga badala yake wafanye kazi kwa bidii ili kuinua elimu nchini.

Pia aliwataka kumkosoa pale wanapoona anakwenda kinyume.

Naye Prof. Joyce Ndalichako alisema wizara hiyo imeachwa kwenye mikono salama, hivyo watumishi wampe ushirikiano wa kutosha waziri mpya.

Ndalichako alimtaka Prof. Mkenda kusimamia vizuri miradi ya elimu ambayo serikali imetoa fedha kwa ajili ya kuiendeleza ikiwamo ya ujenzi wa shule, vyuo na mabweni pamoja na shule za wasichana.

Ndalichako alisema hana hofu na Prof. Mkenda kwa sababu yuko vizuri katika suala zima la elimu.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Rajabu Mabele, alipofika Ikulu, jijini Zanzibar jana, kwa mazungumzo na kujitambulisha. **PICHA: IKULU**

# Mwinyi apongeza ushirikiano JKT, JKU

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amepongeza ushirikiano uliopo kati ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) huku akisisitiza umuhimu wa kuimarisha ili kuleta mafanikio zaidi.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana wakati wa mazungumzo na Meja Jenerali Rajabu Mabele, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), aliyekwenda Ikulu kumsalimia.

Dk. Mwinyi alimweleza Jenerali Mabele kwamba kuna umuhimu wa kuongeza ushirikiano kati ya JKT na JKU hasa katika kuimarisha mafunzo na uzalishaji mali pamoja na mambo mengine hasa ikizingatiwa kwamba JKT tayari imeshapiga hatua kubwa katika kuimarisha miradi ya maendeleo ikiwemo miradi ya ujenzi.

Alisema kwa vile JKT imeanza shughuli hizo kwa muda mrefu na tayari ina uzoefu wa kutosha, ni vyema kwa kikosi cha JKU nacho kikapanua wigo kutoka jeshi hilo ambalo limekuwa likitumiwa katika shughuli mbalimbali nchini hasa za miradi ya ujenzi ambayo mafanikio yake yanaonekana.

Alisisitiza kuwa ni vyema JKU ikajengewa uwezo ili ifike muda iwe na kampuni yake ya ujenzi kama ilivyo kwa JKT ambayo imejijengea sifa kubwa katika shughuli za miradi ya ujenzi nchini.

Rais Mwinyi alieleza kufurahishwa na ukaribu uliopo kati ya JKT na JKU na kueleza haja kwa kikosi cha JKU kuwa na taratibu zote za kijeshi zinazotakiwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ikiwa ni pamoja na kuwa na nidhamu ya kijeshi.

Aliongeza kuwa wakati umefika kwa JKU kuzalisha mali na kujijengea utaratibu maalumu wa kuhakikisha tija inapatikana kama ilivyo kwa JKT.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi alimpongeza Jenerali Mabele kwa kupata wadhifa wa kuwa Mkuu wa JKT pamoja na kupandishwa cheo kuwa Meja Jenerali.

Jenerali Mabele alimweleza Rais Mwinyi ukaribu na ushirikiano uliopo kati ya JKT na JKU, ulioanza mwaka 2001 kwa mwaliko wa sherehe, mafunzo na shughuli zingine za kimaendeleo,

Aidha, Mabele alisema kwa mara ya kwanza SUMA JKT ambayo ni shirika la uzalishaji mali chini ya JKT, limetekeleza mradi wa Tawi la Chuo cha Mwalimu Nyerere visiwani humo mwaka jana kwa ushirikiano na JKU.

Mabele alimweleza Rais Mwinyi kwamba katika uongozi wake ameahidi kushirikiana na JKU ili kuhakikisha inazidi kupiga hatua na kufikia malengo yaliyokusudiwa hasa katika masuala ya uzalishaji, mafunzo na mengineyo.

## Afungwa miaka miwili kujifanya ofisa TRA

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Dodoma, imemhukumu mkazi wa Dar es Salaam, Kitareti Mahuti, kifungo cha miaka miwili jela na kulipa faini ya Sh. milioni mbili kwa kosa la kujifanya mtumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Hukumu hiyo ilitolewa Jumanne wiki hii na Hakimu Mkazi Aloyce Katemana, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa mahakamani hapo na upande wa mashtaka.

Akitoa hukumu hiyo katika kesi namba 170 ya mwaka 2019, Hakimu Katemana alisema mahakama imeridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka, kutoa adhabu hiyo.

Alisema hukumu hiyo imetolewa ili iwe fundisho kwa watu wanaojifanya watumishi wa umma na kutenda makosa hivyo kuharibu taswira nzima ya serikali na utumishi wa umma kwa ujumla.

Awali, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Miyango Kezilahabi, alidai kuwa mshtakiwa alifikishwa mahakamani mara ya kwanza mwaka 2019.

Mwanasheria wa TRA, Hadija Senzia, alidai kuwa mshtakiwa alikuwa akitumia kitambulisho bandia cha TRA, alizunguka kwenye maduka na nyumba za kulala wageni na kujitambulisha kuwa ni mtumishi wa mamlaka hiyo, akiwakagua wateja na kuwatishia kuwapa makosa mbalimbali.

"Document (nyaraka) nyingi zilikuwa za kughushi na alikuwa akiwatishia wale wasiotoa risiti kwa njia ya kielektroniki (EFD) na alikuwa akidai fedha," alidai.

Senzia alidai kuwa mshtakiwa alikuwa akitumia majina tofauti kwenye kitambulisho chake ambacho kilikuwa na namba za kuonyesha kuwa ni mwajiriwa wa TRA na kwamba alikuwa akizunguka mikoa mbalimbali akidai yeye ni ofisa wa kodi akitumia gari aina ya Toyota IST.

"Alikuwa na kitambulisho feki cha TRA chenye jina la Miringe James, kazi ofisa wa kodi," alidai.

# MATANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA KWA AJILI YA HUDUMA YA KUTOA VIFAA VYA KAZI ZA UWANDANI KWA MRADI WA EACOP. KUMBUKUMBU NA: 0010007360

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika Taasisi zenye Weledi na Uzoefu Kuonesha Nia ya Kutoa Huduma ya Vifaa vya Uwandani (Provision of Field Equipment) kwa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini la kusafirisha mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka eneo la Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

Huduma ya Vifaa vya Uwandani Vinavyohitajika ni pamoja na;

- Mahema (Marquee Tents) yenye ukubwa wa saizi ya Kati na Kubwa yenye uwazi wa kufunguka pembeni.
- Viti na Meza za Plastiki na vifaa vya Kutunzia Taka,
- Genereta la Kubebeka kwa Urahisi linatumia petroli lenye ukubwa wa 5KW.
- Nyaya cheneo za umeme zenye urefu wa 5m, 10m na 15m.
- Radio za Mkononi zinazoweza kuchajiwa/Walkie-talkies na vifaa vya kuchajia.
- Sanitiza na Vifaa vya Kunawia Mikono (mobile hand sanitizer).

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Cheti cha Ithibati ya Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Wakala wa Usalama Mahala pa Kazi (OSHA).
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani na sheria za Kitaifa na Kimataifa pamoja na viwango vya Kimataifa vya mafuta na gesi.
- Uthibitisho wa uwepo wa vifaa vya kutosha au uwezo wa kuwa na vifaa katika muda mfupi vinapohitajika.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **9:00** mchana Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **21 Januari 2022.** Kichwa cha Barua Pepe ni 0010007360.

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya Makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA KWA AJILI YA HUDUMA YA UHAMISHAJI NA UHIFADHI WA MAKABURI KWA EACOP. KUMBUKUMBU NA: 0010007361

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika Taasisi zenye Weledi na Uzoefu Kuonesha Nia ya Kuandaa na Kutekeleza Mpango wa Uhamishaji na Uhifadhi wa Makaburi yaliyomo ndani ya eneo (Mkuza) lililoguswa na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki. Mchakato huu utahusisha kuandaa Mikutano na Viongozi wa Mikoa, Wilaya na Serikali za Mitaa Pamoja Kaya zilizoguswa.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini la kusafirisha mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka eneo la Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

Makaburi haya ni yale tu yaliyoguswa na Mkuza wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki katika Mikoa iliyoguswa na Mradi. Mawanda haya hayajumuishi "Maeneo ya Kipaumbele" au kambi na karakana ya kuandalia mabomba pamoja na eneo la kuhifadhi vifaa lililopo ukanda wa bahari katika Rasi ya Chongoleani.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

Huduma za Uhamishaji na Uhifadhi wa Makaburi Utahusisha mambo yafuatayo:

- Kuhakiki maeneo na sehemu makaburi yalipo kama yalivyoainishwa na Mradi.
- Kuandaa Mikutano na Viongozi wa Wilaya na wa Serikali za Mitaa/Vijiji ikiwa ni pamoja na Afisa Afya wa Wilaya ili kuandaa mahitaji yote ya Uhamishaji na Uhifadhi wa Makaburi kwa mujibu wa sheria.
- Kuandaa Mikutano na Kaya zilizoguswa kwa ajili yakuwezesha ufanyikaji wa shughuli za kimila na za kitamaduni pamoja na masuala ya fidia yamelipwa.
- Kuandaa Mikutano na Kaya zilizoguswa pamoja na viongozi wa serikali za Mitaa/Kijiji kwa lengo la kutambua maeneo yakuhamishia makaburi hayo.
- Kushirikiana na Viongozi wa Mitaa/Vijiji kwa ajili ya kutambua vibarua watakaosaidia zoezi la uhamishaji wa makaburi.
- Kuwezesha upatikanaji wa vifaa vyote vya kiafya, kiusalama na kimazingira vitakavyowezesha zoezi la uhamishaji na uhifadhi wa makaburi.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uzoefu wa uhamishaji na uhifadhi wa makaburi nchini Tanzania kwenye maeneo ya viwanda au miradi mingine.
- Uzoefu wa kushirikiana na mamlaka husika kwenye shughuli za uhamishaji na uhifadhi wa makaburi Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Cheti cha Ithibati ya Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Wakala wa Usalama Mahala pa Kazi (OSHA).
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani na sheria za Kitaifa na Kimataifa pamoja na viwango vya Kimataifa vya mafuta na gesi.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **9:00** mchana Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **21 Januari 2022.** Kichwa cha Barua Pepe ni 0010007361.

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya Makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mkenda ameonyesha dhamira katika elimu, aungwe mkono

**MWISHONI** mwa wiki iliyopita, Rais Samia Suluhu Hassan alifanya mabadiliko ya Baraza la Mawaziri kwa kuwateua wapya kuongoza wizara, wengine kupandishwa kutoka unaibu waziri na baadhi kuondolewa kabisa.

Baada ya kuapishwa Jumatatu iliyopita katika Ikulu ya Chamwino, Dodoma, kila waziri na naibu wake wamekuwa wakiripoti katika ofisi zao huku wakiahidi mambo kemkem kulingana na sekta zilizo chini ya wizara hizo.

Miongoni mwa mabadiliko yaliyofanyika, Rais Samia alimteua Prof. Adolf Mkenda, mwanataaluma na nguli wa masuala ya uchumi, kuwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia akichukua nafasi ya mwanataaluma nguli wa elimu, Prof. Joyce Ndalichako, ambaye amekuwa Waziri mwenye dhamana ya kazi na ajira katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

Uteuzi wa Prof. Mkenda ambaye kabla alikuwa Waziri wa Kilimo, nafasi ambayo imechukuliwa na aliyekuwa naibu wake, Hussein Bashe, umeonyesha haukukosewa kutokana na dira yake katika kuboresha sekta ya elimu.

Wakati akikabidhiwa ofisi hiyo, Prof. Mkenda, alisema anatarajia kutafuta wataalamu wabobezi katika elimu, wakiwamo wastaafu ili kupata mchango wao katika maendeleo ya sekta hiyo ikiwamo uboreshaji wa mitaala.

Katika kufanya hivyo, alisema atatenga wiki tatu kuzungumza na watumishi wa wizara na kupitia nyaraka muhimu ili kufanya uchambuzi kuboresha elimu na kwa lengo la kuleta tija kwa maendeleo ya taifa. Mkenda alisema wizara hiyo ni nyeti, hivyo inatakiwa kutendewa haki kwa kufanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na watumishi huku akiweka bayana kwamba si wizara ya kuchezea na kwamba haitakiwi kubadilisha badilisha mambo.

Kwa kauli yake hiyo na mpango wa kuwashirikisha wataalamu wabobezi na magwiji katika elimu, ni dhahiri kwamba amebaini matatizo makubwa yanayo sababisha kudorora kwa elimu na hatimaye kukwamisha mambo mbalimbali kwa maendeleo ya taifa.

Tunasema hivyo kwa sababu yako mambo mengi ambayo yamekuwa yakilalamikiwa katika sekta ya elimu ikiwamo mitaala na kwamba haiendani na muktadha wa sasa wa maendeleo ya sayansi na teknolojia pamoja na kutatua tatizo la ajira ambalo linawakumba vijana wengi ambao wanahitimu katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Aidha, kwa zaidi ya miaka 20 kumekuwa na mabadiliko juu ya mitaala pamoja na mabadiliko ya viwango vya ufaulu ambavyo vimekuwa vikidaiwa kuwa ni sehemu ya mambo yanayoharibu mfumo wa elimu nchini.

Mwaka 2001 kwa mfano, mtu mmoja alipoteuliwa kuwa Waziri wa Elimu na Utamaduni wakati huo, alitangaza kufuta mashindano ya michezo ya shule za msingi (UMITASHUMTA) na ya sekondari (UMISSETA) kwa madai kwamba muda unaotumika kwa michezo hiyo hauna tija katika elimu! Pia waziri huyo huyo alifuta mtaala kwa kuunganisha Kemia, Baiolojia na Fizikia kuwa somo moja na kufutwa masomo ya biashara.

Mwingine aliteuliwa kuwa Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA) na kubadilisha madaraja ya ufaulu kisha kuwa wastani wa ufaulu (GPA) kwa kidato cha pili, cha nne na cha sita. Hii ndiyo maana Prof. Mkenda anaposema elimu si jambo la kubadilisha badilisha mambo, anajua siri iliyoko ndani yake.

Kwa mantiki hiyo anaposema anataka kuwatumia hata wastaafu kupata mawazo juu ya kuleta mabadiliko ndani ya sekta hiyo, Prof. Mkenda anaonekana amedhamiria kuleta mageuzi ya elimu. Kwa hilo anastahili pongezi na aungwe mkono katika azma hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Machinga watafakari, wachukue hatua kuboresha biashara zao

Na Sabato Kasika

**WAFANYABIASHARA** wadogo (Machinga) wameondolewa katika maeneo yasiyo rasmi, katika miji na majiji nchini, kama alivyoagiza Rais Samia Suluhu Hassan, ili wapangwe vizuri waweze kufanya biashara zao bila bugudha.

Dar es Salaam ni jiji mojawapo ambalo lilikuwa na machinga wengi, waliokuwa wakifanya biashara zao katika maeneo mbalimbali yasiyo rasmi, lakini wameondolewa na kupelekwa katika masoko.

Hata hivyo, badala ya kwenda kwenye masoko waliyotengewa baadhi yao wameibuka na mbinu za kujificha vichochoroni wakati wa asubuhi hadi saa 10 jioni, wanaibuka na kurudi kwenye maeneo waliyoondolewa.

Machinga hao ni wa Mbezi Mwisho, wakiwamo wale wenye meza zao, wafanyabiashara kwenye masoko mapya na wengine wanaodai kuwa hawana meza hizo, wote kwa pamoja wamekuwa wakitumia mbinu hiyo.

Kwa mtazamo wangu ni kwamba kupitia mbinu hiyo wanayotumia inaweza kuwakwamisha kupata wateja wa kutosha, pia kukosa sehemu ya kuuzia bidhaa zao na kubaki wakiwa watu wa kutangatanga huku na kule.

Kwanini? Kwa sababu baadhi yao wanakiri kuwa wana meza za biashara katika masoko mpya na huweka vitu vichache, ili waonekane wapo na kisha wanaondoka na kwenda kujibanza vichochoroni.

Wanapoteza muda mwingi wakisubiri ifike jioni warudi kwenye maeneo waliyoondolewa, pia kama wana meza za biashara katika masoko walikopelekwa, inawezekana meza hizo wakapewa wengine.

Kwa hali hiyo ni kwamba, muda wanaoutumia wakiwa mafichoni unapotea bure kwani wanaporudi

**Kwanini? Kwa sababu baadhi yao wanakiri kuwa wana meza za biashara katika masoko mpya na huweka vitu vichache, ili waonekane wapo na kisha wanaondoka na kwenda kujibanza vichochoroni.**

katika maeneo ya awali, wanafanya biashara kwa saa chache giza linaingia wanaondoka kurudi nyumbani.

Hivyo, ingekuwa vyema kama wangetambua hilo kwamba wanaweza kukosa wateja kwani mbinu wanayotumia inaweza isiwe na faida na badala yake wakajikuta wakipata hasara zaidi au kukosa meza katika masoko.

Pamoja na hayo ni vyema pia wakasoma ishara za nyakati, kwani zama zimebadilika, yawezekana wanaamini kwamba, ipo siku watarejea kinyemela kwenye maeneo ya awali na kumbe sivyo.

Ikumbukwe kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla ameshatangaza kila Jumamosi ya kila mwisho wa mwezi, itakuwa siku maalumu ya kufanya usafi kwa wakazi wa mkoa huo.

Ni katika uzinduzi wa mkakati wa usafi na hifadhi ya mazingira wa mkoa huo uliopewa jina la 'Safisha Pendezesha Dar es Salaam', uliofanyika hivi karibuni baada ya kumaliza kazi ya kuondoa machinga kwenye maeneo yasiyo rasmi.

Hivyo, badala ya kufanya biashara kwa kuvizia, njia nzuri ni wao kwenda kwenye masoko huku wakiendelea kudai kile ambacho kwa muda mrefu wamekuwa wakikitaka kutoka manispaa na halmashauri.

Miongoni mwa madai yao ya muda mrefu, ni kuboreshewa miundombinu ya masoko, ikiwamo upatikanaji huduma ya maji, choo, usafiri wa daladala hadi kwenye masoko hayo.

Kimsingi, wao ni watu muhimu ni suluhisho la mahitaji kwa jamii kuanzia yenye kipato cha chini, kati na kipato cha juu na wanatajwa kuchangia katika kukuza pato la taifa, hivyo ni vyema wasiendelee kuhangaika huku na kule.

Badala ya kutumia mtindo huo ambao unaweza kusababisha waendelee kufukuzana na serikali, ni bora wakitulia kwenye masoko yao ili waweze kukuza uchumi wao na hata wa taifa na kusaidia kuondoa umaskini.

# Uongozi SACCOS kuburuzwa mahakamani

**Na Said Hamdani,** LINDI

WANACHAMA wawili wastaafu wa Chama cha Akiba na Mikopo cha Lindi Town Council (LTC), sasa Manispaa, wanatarajia kuuburuza mahakamani uongozi wa chama hicho, kwa madai ya kutolipwa Sh. 9,370,000 zilizotokana na michango yao.

Ndutulu Samike na Simon Msese, waliyaeleza hayo kwa nyakati tofauti, walipokuwa wanazungumza na mwandishi wa habari hizi, ofisi ya Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa (LRPC) mjini hapa.

Wakizungumza wanachama hao wamesema wamechukua uamuzi huo baada ya kuona hakuna matumaini ya kulipwa fedha zao licha ya madai yao kuyafikisha sehemu mbalimbali ya kiuongozi wakiwamo Mkurugenzi, Meya wa Manispaa na Katibu Tawala wa Mkoa bila mafanikio.

Pia walisema walijiunga na chama hicho, Septemba na Oktoba, 2001, wakati huo wakiwa watumishi katika Manispaa ya Lindi na kuchangia Sh. 60,000 kila mwezi kupitia mishahara yao hadi utumishi wa umma ulipokoma mwaka 2017 kwa kila mmoja akichangia Sh. 30,000.

Samike alikuwa mtumishi idara ya biashara, wakati Masese alikuwa idara ya kilimo na kukoma utumishi wa umma mwaka 2017.

Walisema tangu wajiunge na chama hicho cha mikopo miaka 16 iliyopita hawajawahi kupata mkopo licha ya kuomba bila mafanikio.

"Mwaka 2017 utumishi wetu wa umma ulipofika mwisho, tukaomba kulipwa fedha zetu kwani kwa mujibu wa sheria si tena wanachama, hivyo tulipwe chetu lakini hadi sasa bado tunazungushwa tu," walisema. Walisema baada ya kuona usumbufu huo, walilazimika kupeleka malalamiko yao kwa viongozi wa Manispaa husika na hatimaye kwa Katibu Tawala wa Mkoa, kwani ndiye mkuu wa watumishi na kuuamuru uongozi wa manispaa kuhakikisha chama husika kinawalipa wastaafu hao fedha zao kwani ni haki yao kwa mujibu wa sheria.

Pia walisema baada ya agizo la kiongozi huyo wa mkoa kutotekelezwa mwaka 2018, waliuandikia uongozi wa Chama cha Akiba na Mikopo, notisi ya siku 30 iwalipe fedha zao vinginevyo wataufikisha mahakamani iwapo hautatekeleza.

Wanachama hao walisema kutokana na usumbufu wanaoupata hivi sasa, wanakutana na wanasheria wao ili kufungua shauri hilo mahakamani kupata haki yao wanayoidai kwa muda mrefu bila mafanikio.

Katibu Mtendaji wa Chama hicho, Christopher Makwinya, alipotafutwa na mwandishi wa habari kupitia simu yake ya mkononi ili kupata kauli yake, simu ilikuwa imezimwa.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Alan Bukumbi (kulia) na Ofisa Uhamiaji wa mkoa huo, Kamishna Msaidizi wa Uhamiaji, Agnes Luziga, wakiwa na wahamiaji haramu 40 kutoka nchini Ethiopia, waliokamatwa katika Barabara ya Iringa - Mbeya mkoani humo juzi, baada ya kutelekezwa kwenye lori. PICHA: FRANCIS GODWIN

# Walalamikia athari za afya uchimbaji kokoto

**Na Beatrice Shayo**

WAKAZI wa Mbutu Mkwajuni, Wilaya ya Kigamboni, wamesema afya zao ziko hatarini kutokana wa uharibifu wa mazingira unaofanywa na wachimba kokoto na kifusi unaoendelea katika eneo hilo.

Kutokana na tatizo hilo, wameiomba serikali kuwasaidia kuwaondoa wawekezaji hao ambao wanahatarisha usalama wa afya zao kutokana na kuvuta vumbi.

Akizungumza kwa niaba ya wakazi hao, Hassan Mrope alisema mradi huo wa uchimbaji wa kifusi licha ya kuwaathiri wananchi, wawekezaji hao hawasaidii huduma za kijamii inavyotakiwa kama afya, elimu, barabara na maji.

"Hadi sasa hivi tunaelekea mwaka wa nne hatujaona manufaa kwa jamii. Hatujaona chochote kuna baadhi ya nyumba za walimu hazina vyoo. Katika uboreshaji huo tulitegemea mradi ukifika basi wenyeji tupone kwa maana ya kusaidia katika vitu kama ujenzi, ukarabati na mengine," alisema.

Alisema kwa siku yanafika malori hadi 100 na kila lori moja linachukuliwa ushuru kati ya Sh. 15,000 na Sh. 20,000 na fedha hiyo hawaioni katika manufaa ya jamii.

Mrope alisema ukarabati wa barabara hakuna jambo ambalo linawasumbua wananchi magari yanapoita na kujikuta wanaingia vumbi hadi kwenye nyumba zao.

"Hatujaona manufaa kwenye afya katika taasisi ya elimu na mazingira yanazidi kuharibika kutokana na uchimbaji unaoendelea," alisema.

Mrope alisema maeneo hayo wanayochimba kuna baadhi wamenunua kwa ajili ya uwekezaji kuweka hoteli za kitalii leo hali hiyo ya uchimbaji kokote huenda ikasababisha wawekezaji wa ndoto ya utalii ikashindikana.

Alisema kuna athari kubwa inatakiwa kuangaliwa na serikali ili hatua zichukuliwe, ili uharibifu wa mazingira usiendelee na kunusuru afya za wananchi.

"Vibali vyote vinatolewa na manispaa hao wanaohusika na kuangalia mazingira sijui hili linalofanyika huku wanaliona tunachokitaka ni huduma za jamii kama wangetengeneza hii barabara hili vumbi lisingekuwa linatutesa maana hadi ukiwa ndani vumbi linaingia kutokana na malori yanayopita kila siku," alisema.

Pia alisema miradi inavyoletwa katika jamii jambo la msingi iwe inawanufaisha wananchi na sio kuwaathiri kama ilivyojitokeza katika uchimbaji huo wa kifusi.

Alisema kuna waziri ambaye alifika katika mradi huo na kutoa maelekezo kuwa unatakiwa kusitishwa na mpaka sasa hakuna kilichofanyika.

"Huduma za msingi za jamii sio za mtu mmoja mmoja ni za watu wote tunaiomba serikali itusaidie katika hilo na huo uchimbaji wao unahatarisha nyumba zetu," alisema.

Idd Mussa ambaye ni mkazi wa eneo hilo, alisema wamekuwa wakiteseka muda mrefu na vumbi licha ya mamlaka kukaa kimya.

"Athari zipo, lakini mamlaka husika inalifumbia macho jambo hili na sisi wananchi hatuna pa kukimbilia imebidi tuwe wanyonge maana hawa wenye uwezo wana majibu ya mkato," alisema.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Serikali za Mtaa wa Mbutu Mkwajuni, Lucas Katemani, alisema kila jambo lina faida na hasara zake.

"Mfano sisi katika mtaa wetu imesaidia watu kupata riziki zao ndgo ndgo. Kinamama wamekopa mikopa ya halmashauri mategemeo yao ni kokoto na vijana wengi wameanza kujiajiri kupitia hizo kokoto maana wanafanya kazi wanapata riziki na mama lishe nao wanapata riziki wanapouza vyakula huko," alisema.

Katemani alisema athari zipo kwa sababu kuna mavumbi na kuna mashimo makubwa ambayo yanaweza kuharibu mazingira.

"Wanavyochimba ardhi hairudi kama ilivyokuwa lazima iharibike mazingira yanakuwa si mazuri, lakini kuna faida maana serikali inapata kipato kupitia tozo la ushuru linalotokana na kokoto," alisema.

Alisema wanaochimba kokoto ni watu binafsi na zipo kampuni mbalimbali zinakwenda kuchukua vifusi kwa ajili ya ujezi wa barabara.

## Mbunge achangia mil. 28/- ujenzi wa madarasa

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, amechangia zaidi ya Sh. milioni 28 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na vyoo katika shule 18 za sekondari za Manispaa ya Morogoro.

Madarasa na vyoo hivyo ni tofauti na yale yanayojengwa chini ya mpango wa fedha za mradi wa UVIKO-19, ambayo ujenzi wake ulipangwa kukamilishwa Desemba 25, mwaka jana na kuwezesha wanafunzi wote waliochaguliwa kidato cha kwanza Januari 17, mwaka huu.

"Hivi karibuni nilifanya yangu kwenye kata 18 kukagua ujenzi wa madarasa ya mradi wa UVIKO-19, kwa fedha zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan. Nimekutana na matatizo ya hapa na pale ambayo hayahusiani na madarasa ya mradi huu," alisema Abood.

"Changamoto ipo kwa yale madarasa walioanza kujenga wananchi kwa nguvu zao pamoja na vyoo madarasa mengine wanahitaji kumaliziwa hivyo nimeongeza nguvu ili wamalizie na wanafunzi waweze kuyatumia na vyoo mwakani huu," alisisitiza.

Mbunge huyo alisema kutokana na kupokea changamoto zilizotolewa na wananchi, alichangia zaidi ya Sh. milioni 28 kwa kata zenye madarasa na vyoo vilivyoanza kujengwa na fedha hiyo itatumika kwa ajili ya kununua tofali, saruji, masinki ya vyoo na bati.

Naye Ofisa Elimu Taaluma Sekondari Manispaa ya Morogoro, Jaribu Malambughi, alipongeza mbunge kwa kutoa msaada wa fedha za kumalizia vyumba vya madarasa na vyoo vinavyojengwa na nguvu ya wananchi, ili kuondokana na upungufu huo na uhaba wa matundu ya vyoo kwa wanafunzi.

"Nina matumaini yetu sisi uongozi wa Manispaa kuwa misaada hii itawezesha kukamilisha madarasa haya kwa kujengwa kwa wakati na itakuwa na jukumu la halmashauri kumalizia kupaua maboma hayo na jambo hili litaendelea kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani," Malambughi.

Kaimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Kola Hill, Felister Shayo, alisema shule hiyo inahitaji kujengewa choo kingine chenye matundu 30 kwa wanafunzi wa kiume na matundu 35 kwa wasichana kulingana na wanafunzi 1,149 walioko.

Alisema kwa sasa choo kilichoko kina matundu 40 kwa wanafunzi wa kiume na 45 kwa wasichana idadi ambayo hailingani na mahitaji ya sasa.

## Madereva bodaboda walalamikia mikataba

**Na Restuta Damian,** BUKOBA.

BAADHI ya waendesha pikipiki Bukoba, mkoani Kagera, wameomba serikali kuwasaidia kuepuka mikataba kandamizi inayowanyima haki ya manufaa na makubaliano wanayopewa na wamiliki wa vifaa hivyo.

Wakizungumza na Nipashe jana kwa nyakati tofauti, Julius John, Razack Yakub na Salvatory Severine, walisema wengi wanatia saini mikataba pasipo kujua wala kuelewa kile wanachoingia makubaliano nacho.

"Mimi ni mhanga (mwathirika), iliwahi kutokea kwa mmiliki wa awali ilibakia miezi miwili kwa miezi 15 tuliyopangiana, alikuja kuchukua pikipiki yake wakati makubaliano yalisema nikimaliza miezi hiyo nichukue pikipiki iwe mali yangu.

"Visingizio vinakuwa vingi unawaza kwani matatizo anayosema hakuyaona mwanzoni? Nimezalisha pesa kwake kubaki miezi michache ndiyo nionekane kuwa na tatizo. Si haki na hatuna watetezi," alisema John.

Naye Yakub, mkazi wa kata ya Rwamishenye, alisema mikataba mingi inayotolewa na wamiliki inalenga kushindwa lakini kutokana na shida za uchumi inalazimu kutia saini.

Pia alisema na kwenye mikataba hiyo hulazimika kila siku kupeleka Sh. 10,000 bila kujali marekebisho ya kila wiki yanakuwa juu ya mwendeshaji.

"Na kila wiki lazima uende kufanya marekebisho ya sehemu ambayo imeharibika ili kesho uingie kazini, hiyo ni sehemu ya mwendeshaji na si mmiliki ambaye yeye anataka faida. Hajui hicho chombo kinatakiwa kuhudumiwa ili kiingie barabarani," alisema Yakub.

Severine, ambaye ni katibu wa waendesha pikipiki mjini Bukoba, alisema amewahi kupokea malalamiko hayo na kuzungumza na baadhi ya wamiliki ili kuona kama matatizo yanayotajwa yatafanyiwa kazi.

Alisema vijana wanatumia muda mwingi kukimbizana barabarani ili kutimiza mikataba yao ili umiliki wa chombo uwe mikononi mwao lakini inatokea mmiliki anakatisha mkataba au kutotoa kadi ya pikipiki kwa wakati.

"Malalamiko ninayopokea hapa ni kutopewa kadi kwa wakati wanapomaliza makubaliano, kukataliwa mikataba na jukumu la kutengeneza pikipiki pindi inapokuwa imeharibikia ni kwa mwendeshaji," alisema Severine.

Wakili wa Kujitegemea, Jovin Rutainurwa, alisema mikataba huandaliwa na wamiliki wenyewe na wale wanaoingia makubaliano hayo hulazimika kutia saini bila kujua yaliyomo ndani.

"Sheria ya mkataba inasema ukishatia saini lazima mkataba ukubane, hivyo ni vyema kabla ya kufanya hivyo ukajiridhisha kwanza je, utakubali au utakataa?" alisema Rutainurwa.

Hata hivyo, alisema ingewezekana ikawa inatolewa 'ofa' ya kuangalia vipengele vya kubadilishwa ambavyo vitapunguza kumbana mtu lakini mtu akishatia saini lazima atalipa pesa iliyoandikwa kwenye mkataba tu kwa kuwa tayari ametia saini.

# Mil. 170/- kutokomeza ukatili Shinyanga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MFUKO wa Ruzuku wa Wanawake Tanzania (WFT), umetoa Sh. milioni 170 za kutekeleza mradi wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto wilayani Shinyanga.

Mwakilishi wa WFT mkoani Shinyanga, Grory Mbia, alibainisha hayo jana wakati wa uzinduzi wa mradi huo katika hafla iliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wilayani hapo.

Alisema wametoa fedha hizo za ruzuku kwa mashirika saba yakiwamo dawati la jinsia Jeshi la Polisi, Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Shinyanga na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. Kila mnufaika amepatiwa fedha zake na eneo la kwenda kutekeleza mradi huo.

"Matarajio yetu kwenye utekelezaji wa mradi huu, ni kuleta mabadiliko chanya ndani ya jamii, kupunguza ama kutokomeza kabisa matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto," alisema Mbia.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo, Ofisa Elimu Sekondari Halmashauri ya Shinyanga, Stewart Makali, akimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, aliwataka wadau hao kuzitumia fedha hizo kwa malengo yaliyokusudiwa, na kuibadilisha jamii kuachana na matukio ya ukatili.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Deus Mhoja, alisema matukio ya ukatili wa kijinsia wilayani humo yamepungua ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Alitaja matukio ambayo bado yako ndani ya jamii kuwa ni ulawiti wa watoto, ubakaji, vipigo, mimba na ndoa za utotoni, ambayo ndiyo wanashirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kuyatokomeza, yakiwamo mashirika yasiyo ya kiserikali na vyombo vya habari.

Aidha, Ofisa Miradi kutoka Shirika la WEADO, Salome Shangali, alisema fedha hizo za ruzuku ambazo wamepata Sh. milioni 12.4 watazitumia kuyafikia makundi mbalimbali, na kutoa elimu ya kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto ili jamii iishi salama.

Nao waandishi wa habari, ambao ni miongoni mwa wanufaika wa ruzuku hiyo ambao wamepewa Sh. milioni 13.7, waliomba ushirikiano kutoka kwa viongozi wakati wa utekelezaji wa mradi huo, kuanzia ngazi ya kata na wasiwanyime taarifa wala kutopokea simu.

Mradi huo wa kutokomeza matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto wilayani Shinyanga, ulianza Januari mwaka huu, na kuzinduliwa jana, ambapo baadhi ya mashirika yatauhitimisha Machi na mengine Juni, mwaka huu.




Machinga wakiendelea na biashara zao kama kawaida kwenye mitaro ya maji ya mvua licha ya kuondolewa katika eneo la Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Watakiwa kununua ardhi iliyopimwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAKAZI wa Wilaya ya Kibaha wametakiwa kuepuka migogoro ya ardhi isiyo ya lazima kwa kuwa waangalifu wanaponunua ardhi iliyopimwa.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Dagland Consult, Deogratius Nsambo, alitoa ushauri huo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu migogoro inayoweza kuepukika kwa kununua ardhi iliyopimwa.

Nsambo alisema katika kufanya kazi zao za mambo ya ardhi wamekuwa wakikumbana na migogoro inayotokana na baadhi ya wananchi kununua ardhi ambayo ambayo haijapimwa.

"Watu wanaouziana kienyeji ndiyo wanaochangia kuendelea kuwapo kwa migogoro, wananchi wanatakiwa kubadilika na kuanza kupima maeneo yao na wale ambao wananunua wazingatie maeneo yaliyopimwa," alisema.

Alisema kupima ardhi kuna faida kubwa licha ya kuondoa migogoro ya ardhi pia inasaidia kutumika kama dhamana kwa ajili ya kukopa fedha kwenye taasisi za fedha.

Kwa mujibu wa Nsambo, ardhi ambayo imepimwa inakuwa inatambua mipaka ya kila eneo hivyo hata kuingiliana kwenye mipaka siyo rahisi tofauti na ile ambayo haijapimwa.

"Tunatoa elimu kuhusiana na ardhi ya umiliki wa ardhi kwa wananchi kwenye mikutano ya mitaa au mikutano mbalimbali ya kijamii na tunawashauri wananchi kabla ya kununua ardhi iwe kisheria au kienyeji waende halmashauri ili kuyatambua maeneo hayo ili kutonunua sehemu ambazo hazijapangwa kwa ajili ya makazi," alisema.

Alisisitiza kuwa kununua ardhi ambayo hawajaihakiki inaweza kuwasababishia kununua maeneo ambayo tayari yana umiliki na kusababisha kuzalisha migogoro inayoweza kuepukika.

HABARI KITAIFA

# RC aonya ujanja mikopo halmashauri

**Na Neema Hussein,** MPANDA

MKUU wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, amewaonya viongozi wa serikali katika mkoa kutojihusisha na udanganyifu wa mikopo inayotolewa kwa vikundi mbalimbali.

Udanganyifu huo ni pamoja na baadhi ya viongozi kumiliki vikundi hivyo kama ilivyokuwa kipindi cha nyuma.

Mrindoko alitoa onyo hilo jana wakati akikabidhi mikopo ya asilimia 10 kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika. Alisema vijana waendelee kujitokeza kwa wingi kuchangamkia fursa za mikopo ili kujiajiri na kuacha kuzurura ovyo mtaani huku akisema idadi ya vikundi vya vijana na wenye ulemavu waliojitokeza katika mikopo hiyo ni ndogo kulinganisha na wanawake.

"Mikopo hii mliyoiomba mkaitumie kwa malengo yaliyokusudiwa na si vinginevyo. Mikopo hii ni haki yenu msiende kuwapa viongozi wanaowarubuni kuwa wamewapigania mkapata. Hakuna aliyewabeba na kama kuna kubebana basi aliyewabeba ni Rais Samia Suluhu Hassan na hakuna mwingine," alisema.

Mrindoko aliwataka wakurugenzi wa halmashauri zote za mkoa wa Katavi, kusimamia vikundi vilivyopewa mikopo na kuhakikisha vinapewa elimu kulingana na biashara zinazofanywa na vikundi husika ili kuepuka kudumaa kimaendeleo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, Shabani Juma, alisema wametoa mikopo ya zaidi ya Sh. milioni 200 na wanawake wenye vikundi 11 watapata Sh. 157,790, 000.

Juma elisema vikundi vya vijana vitapata zaidi ya Sh. milioni 75 na watu wenye ulemavu watapata Sh. milioni 10. Mikopo hiyo inatokana na asilimia 10 ya mapato ya robo hii ya pili ya halmashauri ambayo ni zaidi ya Sh. bilioni mbili.

Alisema wamejipanga kutoa elimu zaidi kwa vikundi ili kuhakikisha wanainua kipato na uchumi wa wananchi wa Tanganyika, hivyo kurudisha mikopo hiyo kwa urahisi zaidi.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Tanganyika, Halima Kitumba, alisema vikundi vingi vya vijana ni vya ujanja ujanja ambavyo wakijiandikisha siku ya kwenda kukagua wanabaini upungufu mwingi.

Baadhi ya wanufaika wa mikopo hiyo, wakiwemo Masoud Mussa na Anna Peter, walishukuru serikali kwa kuwapatia mikopo hiyo huku wakiahidi kuitumia kwa kazi walizokusudia ili kujikwamua kiuchumi.




Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Kidigitali wa Vodacom Tanzania, Goodluck Moshi (kulia), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa mshindi wa promosheni ya Vodacom Tusua Mapene, Lilian Haule, mkazi wa Tegeta, katika hafla iliyofanyika kwenye viwanja vya Mbagala Zakhem, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Vikwazo elimu Lindi vyatajwa

**Na Said Hamdani,** LINDI

IDARA ya Elimu mkoani Lindi imetaja vikwazo 16 vinavyokwamisha kufikia malengo iliyojiwekea katika taaluma, hivyo kusababisha wanafunzi kushindwa kufanya vizuri kwenye mitihani ya taifa.

Baadhi ya vikwazo hivyo ni pamoja na wanafunzi kutofahamu vizuri masomo ya Kingereza, Hisabati kwa shule za msingi, Fizikia na Kemia kwa sekondari.

Hayo yamebainika wakati wa mkutano wa tathmini uliofanyika Ruangwa, uliojumuisha wataalamu wa elimu ngazi ya mkoa, maofisa wilaya, wadhibiti ubora elimu, wakuu wa shule za sekondari na msingi, wakurugenzi wa halmashauri na kubatizwa jina la 'Maabara ya Elimu'.

Akisoma taarifa ya tathmini ya elimu kwa mkoa, Ofisa Elimu Taaluma, Janet Moyo, alisema kiwango cha somo la Kiingereza kwa shule za msingi hakiridhishi na ufaulu wa Kiingereza kwa sekondari uko chini kwa ujumla hakifanyi vizuri.

Moyo alitolea mfano wa mwaka 2021 kwamba hali ya ufaulu kwa somo hilo ulikuwa daraja E.

Kuhusu Hisabati, Moyo alisema mkoa haukufanya vizuri baada ya kupata wastani chini ya asilimia 50, huku wanafunzi waliopata alama 'A' wakiwa asilimia 10 tu, wakati masomo ya Fizikia na Kemia nayo hayafanyi vizuri.

Kutokana na taarifa hiyo, mkutano huo umetaja masomo matano likiwamo la Kiingereza kwa shule za msingi, Hisabati, Fizikia na Kemia kwa sekondari kuwa miongoni mwa changamoto kubwa zinazohitaji mkakati madhubuti ili kuhakikisha hali hiyo ya sasa inaondoka katika elimu mkoani Lindi.

Katika kushughulikia tatizo hilo, Ofisa Elimu Mkoa wa Lindi, Vincent Kayombo, ameamua kuunda jopo maalum la wataalamu wa udhibiti ubora na wakuu wa shule ambao amesema tayari wameainisha kila somo na hatua ambazo zimetakiwa kufikiwa kila mwezi.

# DC kukamata wazazi, walezi wasiopeleka watoto shuleni

**Na Ashton Balaigwa,** KILOSA

MKUU wa Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro, Alhaji Majdi Mwanga, ametishia kuwakamata na kuwafikisha mahakamani wazazi na walezi watakaoshindwa kuwapeleka shuleni watoto waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza.

Mwanga alisema hayo mjini hapa katika mkutano wa hadhara na wananchi kuhusu uhamasishaji shughuli za maendeleo ikiwamo sekta ya elimu.

Alisema ili kuhakikisha watoto wote waliochaguliwa kidato cha kwanza wanaingia madarasani Januari 17, mwaka huu, ofisi yake imeandaa mikataba kati ya wazazi, walezi kuhusu kudhibiti tabia ya baadhi ya wazazi kuwa chanzo cha wanafunzi kukatisha masomo.

Alisema hatua hiyo ni kutekeleza ibara ya 11 (2) na (3) ya Katiba inayosisitiza haki ya msingi ya kupata elimu.

"Tumeshatayarisha mikataba ambayo inalenga kuimarisha usimamizi kwa wazazi na walezi, kutimiza wajibu wa malezi kwa watoto wao na ilishasambazwa katika shule za sekondari na ofisi za serikali za vijiji na kata," alisema.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kilosa, Ameir Mbaraka, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha Wilaya ya Kilosa Sh. bilioni 4.3 zilizotumika kwenye ujenzi wa vyumba 186 vya madarasa.

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya wilaya hiyo, Kisena Mabuba, alisema jumla ya wanafunzi 9,405 ambao wanatarajia kuanza masomo ya kidato cha kwanza Januari 17, mwaka huu.

Mabuba alisema mpango mwingine ni kuhamasisha uandikishwaji wanafunzi wa awali na darasa la kwanza kutoka kwenye jamii za wafugaji.

"Nawataka jamii ya wafugaji wajitokeze kuwaandikisha watoto wao waliofikia umri wa kuanzikishwa shule ili waepuke mkono wa sheria," alisema Mabuba.

Pia alisema halmashauri itaendeleza mchakato kusajili shule shikizi, ili kutoa fursa kwa wanafunzi wa shule za msingi kuondokana na ulazima wa kutembea umbali mrefu.




Mama kafagia ndani, huenda kasahau mabuibui darini




BUFE

IJUMAA JANUARI 14, 2022

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

SHULE J3; HITAJI RASMI SH. 980,000; KASAIDIWA SH. 45,000

# Walezi bibi & babu hawana hata senti, binti kafaulu 'A', shule vipaji maalum

• Baba kawatelekeza, mama katoweka, wadogo zake 2

**Na Christina Mwakangale**

MARA zote kuna usemi wa kijamii, safari ya maskini ni mtihani mgumu kufanikiwa. Kila panapofunguka mafanikio, umaskini huvuta nyuma safari hiyo. Hebu fuatilia mkasa huu:

Bahati Ngolikwa (14), ni binti aliyehitimu darasa la saba kwa mafanikio makubwa sana, licha ya wazazi kuwatelekeza na wadogo zake na hawajui waliko, huku babu na bibi yake wana maisha duni.

Lakini hilo halijawahi kumkatisha tamaa katika taaluma maishani, bidii na nidhamu shuleni iko dhahiri, hata shuleni wakamheshimu na kumpa cheo cha kiranja mkuu, awe kioo cha wenzake.

Binti huyo akiwa mhitimu kutoka Shule ya Msingi Juhudi, iliyopo katika Halmashauri ya Mbeya Vijijini, sasa furaha yake ya kufanya maajabu katika mtihani wa mwaka jana, inaingia dosari anakwama mahitaji ya kifedha kumwezesha kujiunga na sekondari kutimiza ndoto yake kielimu.

"Nilijisikia furaha kubwa nilipochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka wa masomo 2022. Changamoto ni malipo ya ada nilikochaguliwa," anasema Bahati, mwenye ndoto ya kuwa daktari wa binadamu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Sauti ya Mama Africa Foundation (SAMAFO), Tabitha Bugali,



Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Sauti ya Mama Africa (SAMAFO), Tabitha Bugali, akimkabidhi vifaa vya shule Bahati (kushoto), vikiwamo madaftari 14, mkebe, kalamu 12. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

anaiambia Nipashe wiki hii baada ya kufika nyumbani kwa walezi wa binti huyo na kukabidhi vifaa vya shule, anawaomba wadau wa maendeleo waungane kufanikisha elimu ya Bahati.

Anasema Bahati amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Galijembe - Vipaji Maalum iliyoko katika Halmashauri ya Mbeya Vijijini, lakini ana changamoto ya kujiunga na shule hiyo kutokana na kukosa pesa na kuishi bweni.

"Anaishi na babu yake Simon Ngolikwa na bibi yake Agnes Samson, kitongoji cha Iwindi, Kata ya Iwindi, Halmashauri ya Mbeya Vijijini. Inasemekana baba hajulikani, ana (Bahati) wadogo zake wawili nyuma yake.

"Mama yake naye aliwatelekeza hao watoto, babu yao anasema hajui alipo mama yao. Mahitaji ya Bahati shuleni alipochaguliwa ni zaidi ya Sh. 900,000 ambayo ni ada, bweni na chakula, ambayo walezi wake hawana. SAMAFO tumetoa msaada wa vitabu vya thamani ya Sh. 45,000," anasema Tabitha.

**BIBI AFUNGUKA**

Bibi wa Bahati, anayeitwa Agnes anafafanua: "Binti huyu ni wa kukaa nyumbani kufanya kazi za nyumbani akitoka shuleni. Hajawahi kushindwa kwenda shuleni hata siku moja bila ya sababu, yaani sio wa kuhangaika.

"Amemaliza shule yake amefaulu, sasa uwezo wa bibi yake sina. Yeye anapenda shule, nilifurahi sana, sikutegemea, nikaona amefaulu sasa uchumi mgumu."

**KUTOKA SHULENI**

Mwalimu wa Taaluma Shule ya Msingi Juhudi, Fred Charles, anamwelezea Bahati kuwa mwanafunzi aliyekuwa na bidii darasani;

"Kama mwalimu wa darasa na taaluma, tumekuwa naye tangu muda, uwezo wake wa kitaaluma tangu akiwa darasa la tano, sita...kwa kweli anajitahidi kimasomo pamoja na changamoto, anaweza kushika nafasi ya kwanza kwenye mitihani kata nzima.

"Tulianza kumfuatilia tangu mapema tukampa nafasi ya uongozi ya dada mkuu. Aliongoza vizuri na kushawishi mabinti wenzake kusoma na kutojiunga makundi mabaya na katika asasi za haki za binadamu huwa anazungumza kuhusu haki za wasichana.

"Changamoto za kiuchumi kwenye familia yake, lakini hajakata tamaa. Kama walimu pamoja na Mwalimu Mkuu tuliendelea kutafuta msaada ili asome," anasema Mwalimu Charles.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Juhudi, Erasto Peter, anasema: "Mwaka wa masomo 2021 wanafunzi wote 54 walifaulu, wamepata asilimia 100 kwenda sekondari na shule yetu ni ya sita.

"Waliochaguliwa kwenda vipaji halmashauri ni wawili wanatoka shule hii ya Juhudi na kata hii akiwamo Bahati, ambaye ana wastani wa 'A'.

"Ingawa hana uwezo wa kumpeleka kwenye shule aliyopangiwa, baada ya kufuatilia na kugundua gharama ni takribani Sh. 980,000 kwa mahitaji yote ya msingi," anahitimisha Erasto - Mwalimu Mkuu.

• ***Kwa mwenye msaada wasiliana na fa-***

UCHUMI

# Ijue siri ya ombaomba barabarani na mtandao mpana, watoto hadi wazazi

- Wazee wasioona wanaazima watoto kuwasaidia
- Wazazi wanajificha, jioni huibuka kukusanya pato
- Jijini Dar kambi yao ya makazi imejikita Kigamboni
- Kinamama 'huzuga' barabarani wakifuatilia watoto

**Na Beauty Mwakatobe, TUDARCO**

TATIZO la ombaomba jijini Dare es Salaam na huenda miji mingine mikubwa nchini ina sura ya 'donda ndugu', maana kona nyingi na maarufu jijini zinatawaliwa na ombaomba, wengi wakiwa watoto wanaopaswa kuwa shule za msingi.

Hapo inarejewa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 ambayo inamtafsiri mtoto kuwa "Mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka kumi na nane" na ina ufafanuzI "Itakuwa ni wajibu wa mzazi, mlezi au mtu mwingine yeyote anayemlea mtoto kumtunza mtoto huyo..."

Katika hilo, Sheria hiyo inaorodhesha haki za msingi

anazotakiwa kupatiwa mtoto kama za chakula, malazi, mavazi, huduma ya afya pamoja na kinga, elimu na

muongozo, uhuru na haki ya kucheza na kupumzika.

Aidha, Sheria ya Elimu nchini, inaainisha wajibu wa mtoto kupelekwa shule ni lazima.



Watoto wanaoshughulika kuomba mtaani katika nyendo zao.

**NINI KINAENDELEA MTAANI?**

Jijini Dar es Salaam, kuna baadhi ya maeneo yanayoonyesha watoto wa mtaani wakizurura kuomba kwenye foleni za magari na sehemu za biashara za watu.

Hapo kuna suala kukutwa wamezagaa watoto kwenye sehemu zenye taa kama vile Mwenge na Ubungo jijini Dar es Salaam, hali kadhalika Daraja la Salender, katika barabara ya Ali Hassan Mwinyi.

Utafiti wa Nipashe kupata undani wa suala hilo kwa siku kadhaa, umegundua watoto hao wa mtaani kwa sehemu kubwa wanatoka mkoani Dodoma na makazi yao jijini Dar es Salaam, ni eneo la Tungi, Kigamboni, ambako vyumba vinapangishwa gharama nafuu.

Pia, Nipashe imebaini kwamba asilimia kubwa ya watoto hao wanafuatana na ama wazazi au walezi wao katika maeneo hayo katika shughuli za kuomba barabarani.

Baadhi ya wazazi au walezi wa watoto hao, wakiwa barabarani hudanganya kuwa wanauza karatasi za kujifutia maarufu 'tishu' au bidhaa zingine ndogo, lakini Nipashe imebaini lengo kuu ni kufuatilia nyendo za watoto hao katika kuomba.

Pia, imebainika mbinu nyingine kuwapo baadhi ya wazazi au walezi wanaowatumikisha watoto wao kuwatembeza wazee walemavu kuomba barabarani, huku wakiwafundisha watoto hao mbinu za kusema uongo wanapodadisiwa uasilia na undani wa maisha yao, lengo kuu ni kuficha ukweli namna watoto wanavyotumikishwa.

**UNDANI WA WANAVYOISHI**

Mwandishi wa makala hii alikutana na changamoto hiyo, akiwa na ushuhuda wa pale alipokutana na binti ambaye alidanganya juu ya uasilia wa hali ya nyumbani kwao, kwamba aliyefuatana naye ni dada yake.

Kupitia maelezo ya watoto wawili, binti mwenye umri wa miaka 13 alijitambulisha kwa jina Elizabeth na kijana wa kiume mwenye umri wa miaka saba, anayejitambulisha Joseph, wanatoa ufafanuzi, mtaani Mwenge wakiongozana na mzee mlemavu wa macho, wametoa sababu za wao kuwa mtaani kuomba.

Mosi wanataja, wameingia katika maisha ya kuomba, baada ya mama yao kugongwa na pikipiki na kuumia mguu, hata kumfanya asiweze kutembea tena,

Katika hilo wanaorodhesha gharama za kumudu maisha, ikijumuisha pesa ya kumtibu mama yao mgonjwa wa miguu, pia pesa za kulipa kodi ya chumba wanachoishi na chakula, huku wengine wengi nao wakiangukia hoja ya umasikini uliojikita kwao.

"Natamani sana kusoma ili nije kuendesha ndege nikimaliza masomo yangu" anasema Joseph anayetaja changamoto zinazowakuta ni pamoja na kuzunguka na jua barabarani, wananusurika kila mara kugongwa na bodaboda, kushambuliwa na matusi wanapoomba kwenye magari.

**MZEE ANAYEOMBA**

Mzee anayefuatana na watoto hao, anaanza kujitambulisha asili yake mkoani Dodoma, ila sasa anaishi Kigamboni Shimoni, anaanika ukweli kwamba watoto anaoambatana nao, haishi nao, bali huwa anawachukua mikononi mwa wazazi wao akiomba wafuatane kwenye 'kibarua' chake cha matembezi ya kuomba brabarani.

Kwa mujibu wa mzee huyo, huwa hafuatani nao kila siku, bali ana utaratibu wa kuomba watoto tofauti kutoka mikononi mwa wazazi wao wakamsaidie kwenye 'kibarua' cha kuomba, akipewa sharti la kuwa makini kuwatunza na kuwarejesha salama.

WANANCHI WANENA

Mchuuzi mmoja katika eneo la Mwenge, barabara ya Coca Cola, ambaye hakuwa tayari kutaja jina lake, ila ni mwelewa wa undani wa maisha ya watoto hao wanaoomba, anasimulia kwamba huwa wanatumikishwa na kuna watu wanaowaleta maeneo hayo na baadaye wanawafuata kukusanya pesa walizokusanya watoto hao.

"Nimeshuhudia kwa macho yangu hapa mataa ya Mwenge, mama mmoja anachukua kwa baadhi ya watoto wanao omba omba, lakini kwa sababu mimi sina sheria ya kumhoji kwanini anawatumikisha watoto hao sikuweza kufanya chochote" anasimulia mtu huyo.

**SHERIA INAVYONENA**

Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 na marekebisho yake ya Mwaka 2014, ina ufafanuzi kuhusu ajira ya mtoto:" Mtu hatamuajiri au kumfanyisha mtoto kazi ambazo zinaweza kuwa na madhara kwa afya, elimu, akili, mwili au kwa maendeleo ya kimaadili ya mtoto".

Ni ufafanuzi wa kisheria unaoanika namna halisi ya mtoto kuomba, inakinzana na sheria hiyo, katiba ya nchi, pia Sera na Sheria ya Ellimu, inayowataka watoto hao kuwa masomoni, kwani elimu ya msingi ni ya lazima na umri wao unaelekeza wangekuwa huko.

Pia, ikirejewa sheria hiyo ya mtoto kuna ukiukwaji juu ya hali zake kwa kuwekwa katika mazingira hatarishi barabarani kama walivyoshuhudia wenyewe katika mazungumzo na Nipashe dhidi ya ajali kugongwa barabarani, mazingira hatarishi, kuchangamana na makundi yenye maadili mabaya na ni muda anaotakiwa kuwa shuleni.

**HATUA ZA SERIKALI**

Msuguano wa kiserikali na matendo ya kuomba jijini Dar es Salaam yamedumu muda mrefu zaidi, katika awamu tofauti za uongozi wake.

Mnamo Mei 21 hadi 27 mwaka jana, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, katika nafasi tofauti ametamka hatua za kushughulika na ombaomba waliozagaa mkoani humo, pale alipoahidi mwisho wao ni mwezi Juni, kwamba watasafirishwa kurejeshwa makwao, hatua ambayo ilishawahi kuchukuliwa huko nyuma.

Ni vita aliyoanzisha mkoani dhidi ya ombaomba, akiagiza viongozi wa wilaya na halmashauri kuratibu mchakato wa kuwaondoa na kuwarejesha makwao, huku wenyewe 'wakijibu mapigo' kwamba 'hawako tayari.'

Makalla alipokutana na wadau mbalimbali kwa lengo la kuweka mikakati dhidi ya ukatili wa watoto, akatumia fursa hiyo kuzungumzia usugu wa ombaomba wanaofanya hilo kama mradi wa kuwapatia kipato.

Makalla si kiongozi wa kwanza wa mkoa huo kuanzisha operesheni ya kuwaondoa ombaomba katika mkoa huo, ilishawahi kufanywa na wakuu wa mikoa kadhaa waliomtangulia bila mafanikio akiwamo Yusuf Makamba,

aliyejaribu kuwarudisha ombaomba makwao, lakini baadaye walirejea baada ya muda mfupi walipoondolewa jijini .

Baadaye Makamba, akabadili mkakati akiwaruhusu kurudi jijini, lakini kwa kuzingatia sheria na kanuni stahiki, huku Paul Makonda, mtangulizi wa Mkuu wa Mkoa Makalla, naye alibuni operesheni, ambayo nayo ikafifia.



Mtu mzima, akiambatana na mtoto kuomba barabarani. **PICHA: MAKTABA.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Mama kafagia ndani, huenda kasahau mabuibui darini






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

SIKU moja mama alirudi nyumbani jioni na kuingia chumbani mwake, ghafla alitoka amekasirika na kutufokea, huku akihoji wakati hayupo nani aliingia chumbani mwake, huku akitishia kutuchapa.

Tulitazamana tusijue la kufanya na yawezekana na kati yetu mmoja aliingia chumbani humo, lakini hatukujua nini kilikuwa kimejiri, mpaka kumkasirisha mama kiasi hicho, hivyo tukajiandaa kwa lolote.

Mama alipoona hampati mbaya wake, ikabidi afunguke kuwa amekuta ndani kuna mchanga na takataka zingine kutoka nje, zikionyesha dhahiri kuna mtu aliingia bila kuvua viatu na kuacha uchafu huo chumbani.

Kwa kuwa na huruma aliona isiwe taabu, basi akachukua fagio na kuingia kusafisha na kuondolea mbali uchafu ule wa mchanga na majani majani na kutuonya tusirudie ujinga ule.

Tukashukuru tumepona na kuendelea na michezo yetu. Kwa kweli mama alikuwa mwanamke hasa hatujapata kuona, hakutaka kuona chumba chake kimechafuliwa hata siku moja. Alituzuia kuingia chumbani mwake kama hayupo, isipokuwa akiwa ametuita kututuma mahali na si kwenda kusogoa.

Lakini, wakati amemaliza kufagia, ghafla nje tukaona ameokota vijiti viwili na kuingia navyo ndani. Tulitaka kumuuliza kwa nini uchafu ule alikuwa akiurudisha ndani, tukasita. Lakini, kaka yetu jeuri hivi akajitosa kumuuliza.

Mama kwa kuchelea kueleweka vibaya nasi wanawe, akapiga moyo konde na kutuambia kuwa kama si vile vijiti tusingekuwa tulivyo. Tulielewa kuwa kumbe ile ilikuwa ni kinga.

Kwani alisema aliachiwa na marehemu bibi yetu. Yalikuwa ni mambo ya jadi, kwamba kumbe vile vijiti vilikuwa muhimu sana kwa maisha yetu.

Akatuasa tusiyaseme nje, kwamba ana vijiti vinatulinda asingeeleweka kwa majirani zaidi ya kuonekana kigagula. Tukanyamaza ikawa siri yetu.

Lakini, jambo moja ambalo lilitushangaza baada ya kunong'onezana, tulichokiona chumbani kwa mama siku hiyo hiyo, ni kwamba alikuwa amefagia vizuri sakafuni, lakini akasahau darini kulikojaa matandabui.

Nami nikauvaa ujasiri na kumuuliza mama, kwa nini alifagia sakafu akaacha matandabui darini? Alitazama juu na kutikisa kichwa kuonyesha kuwa tumemwaibisha, akasema tu kwa geresha, kuwa alishayaona na alikuwa anajipanga kuyaondoa.

Sasa Chifu Hangaya kaamua kuwasambaratisha kwa kufagia chumbani, lakini huenda kasahau darini, penye mabuibui, si ajabu akarudi kusafisha.

Wale waliokuwa wakikimbilia mbio za urais mwaka 2025 kwa mujibu wa maelezo yake, ni sawa na ule mchanga ulioingizwa chumbani kwa mama, lakini akakumbuka kuna vijiti viwili, wazee wenzake anaowabakisha kuweka sawa nyumba na familia, iwapo ulinzi wa hakikka na ubora wa kifamilia.

Chifu Hangaya alipoona wanawe tunamwangalia

kwa jicho la mshangao kuwa alishasema hao ni wale aliosema awateme ili wapate muda wa kujipanga kwa ajili ya kinyang'anyiro, lakini kumbe kuna wawili alioachiwa na bibi yetu, amewabakiza kundini.

Akasema hawa ni kaka zangu, lazima niwavute pale maeneo, ili wamsaidie kuwaweka sawa 'mabarobaro' aliowateua kushika nafasi ya juu, katika serikali yake, kwa sababu anajua walivyo machachari anawadhibiti wasipandishe mabega, kuanza kusakama wananchi, badala ya kuwasaidia.

Sasa mlioteuliwa na kuapishwa pale Ikulu Chamwino, Dodoma angalieni Mama, si ajabu anarudi ndani kuondoa na kupukuta mabuibui aliyoyasahau. Shauri yenu mkilikanyaga mmekanyagwa. Mkimzingua Chifu Hangaya hakawii kukuzingueni. Shauri yenu. Alamsiki!

BIASHARA

MENEJA TARURA:

# Haya hapa maisha mapya ukusanyaji ushuru wa maegesho magari jijini Dar

## • Kumebainika udokozi, dawa iko jikoni



Mtoza ushuru katika Jiji la Dar es Salaam, akipiga picha gari kwa ajili ya kuliingiza katika mfumo wa ulipaji ushuru wa maegesho kidigitali. **PICHA: MTANDAO**

**Na Maulid Mmbaga**

MFUMO mpya wa kidigitali wa ukusanyaji ushuru wa maegesho ya magari unaotumika mkoani Dar es Salaam, unatajwa kuzaa matunda idadi ya mapato yanayotokana na makusanyo hayo, kuongezeka na kuinufaisha serikali.

Katika Mkoa wa Dar es Salaam mfumo huo wa ukusanyaji ushuru kidigitali unaoratibiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) ulianza rasmi Desemba Mosi 2021 na unatajwa kuwa na mafanikio kutokana na kusaidia katika kuzuia upotevu wa mapato.

mfumo huo.

Awali ukusanyaji ushuru wa maegesho ya magari ulikuwa ukiendeshwa kwa mfumo wa kutoa risiti za kawaida 'risiti za kitabu' njia inayodaiwa kuwa na mianya mingi ya upotevu wa mapato serikalini, kutokana na baadhi ya watumishi wasio waaminifu kuutumia kama kichochoro cha udanganyifu.

Kwa Mkoa wa Dar es Salaam, mtumiaji wa maegesho anatakiwa kulipa Sh. 500 kwa saa na Sh. 2,500 kwa siku kutoka 4,000.

**MAFANIKIO YA MFUMO**

Meneja wa Wakala wa Barabara wa Mijini na Vijijini

(TARURA) Mkoa wa Dar es Salaam, Geofrey Mkinga, anabainisha kuwa mfumo huo wa ukusanyaji ushuru wa maegesho ya magari kidigitali, unawawezesha kukusanya zaidi ya Sh. milioni 32 kwa siku, huku kiwango cha makusanyo yakitarajiwa kuongezeka.

Anasema mfumo huo mpya wa ukusanyaji mapato ni muhimu katika kuzuia kuvuja kwa mapato, hali inayodhihirika baada ya kuanza rasmi kwa matumizi ya mfumo huo ambao mapato yanayokusanywa yanaonekana.

"Katika jitihada za uelimishaji hadi sasa tumeyafikia makundi mbalimbali na kuyaongezea uelewa na elimu juu ya mfumo huo wa ukusanyaji wa mapato kidigitali," anasema Mkinga.

Anakumbusha kuwa katika mfumo huo mmiliki wa chombo cha usafiri anapaswa kulipa ushuru wa maegesho kidigitali baada ya kupatiwa namba ya malipo (control number) na atatumia kumbukumbu hiyo kulipia huduma hiyo, kwa kutumia mtandao wowote wa simu au benki za NMB na CRDB, au kupitia mawakala wa huduma za fedha.

Rai yake ni kwa watoa huduma za maegesho zaidi ya 900 katika mkoa huo kujiepusha na udanganyifu na kutoa lugha chafu kwa wateja, akitahadharisha watakaobainika kukiuka taratibu za ukusanyaji mapato, wataondolewa kazini.

**MIONGOZO ILIVYO**

Aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, alishatamka kwamba mtumiaji maegesho atatakiwa kulipa ushuru ndani ya siku 14 badala ya siku saba tangu alipotumia maegesho.

Waziri huyo amefafanua kuwa endapo atashindwa kulipa ndani ya muda huo, atatakiwa kulipa ushuru wa maegesho pamoja na faini ya Sh. 10,000 badala ya Sh. 30,000 zilizokuwa zilitozwa awali, baada ya kufuta adhabu za kiwango hicho cha fedha.

Anaeleza kuwa, miongoni mwa changamoto wazozifanyia kazi ni pamoja na wateja kupatiwa taarifa za kudaiwa ushuru wa maegesho kwa wakati, kupunguza gharama za maegesho, kuongeza muda wa kulipa ambao awali mtumiaji maegesho awali alitakiwa kulipia ndani ya siku saba tangu alipotumia maegesho.

Mkinga anasema, wamebaini udanganyifu unaofanywa na baadhi ya wakusanya ushuru na wateja wanaotumia huduma hiyo. Baadhi ya wakusanya ushuru hufanya mazungumzo haramu na wateja wao wakilipana fedha nje ya mfumo ambazo hazifiki ofisini.

Anasema, baadhi ya wenye magari nao 'hubambikiwa' madeni baada ya wakusanya ushuru kuyapiga picha magari na kuyaingiza kwenye mfumo kuwa yanadaiwa, katika maegesho ya TARURA.

Mkinga anafafanua: "Wanamwambia mteja tupe 'buku' (Sh. 1000) ili asiipige picha gari yake kwa ajili ya kuiangalia na kuingiza katika mfumo wa malipo kwa njia ya mtandao.

"Kufanya hivi ni kuikosesha mapato serikali na kuwaingiza kwenye madeni wasiostahili, tumeshaijua hii mbinu baada ya kupata taarifa kutoka kwa wateja wema."

**HATUA ZILIZOCHUKULIWA**

Meneja huyo wa TARURA anaeleza katika kulishughulikia hilo wanashirikiana na mzabuni na wamewaondoa baadhi yao wamethibitika kujihusisha na udanganyifu huo katika vituo vyao vya kazi kwenye maeneo ya Posta kuelekea Feri-Kigamboni, jijini Dar es Salaam.

Maeneo mengine walipoondolewa ni katika vituo vyao ni Kariakoo, Millenium Tower na Lumumba, akidai wanawafahamu baadhi ya wakala hawaupendi mfumo huo, kwasababu hauwapi mianya mingi ya kufanya udanganyifu.

Anaeleza, katika kukomesha vitendo hivyo, TARURA imeunda mkakati na timu ya wataalamu, inayofanya tathmini na usimamizi kwa kupita katika maegesho yao yote ili kubaini vyombo vya moto ambavyo havijaingizwa kwenye mfumo wa ulipaji.

Pia anadokeza TARURA imebaini kuwapo vitendo hivyo, baada ya kupata taarifa zenye ushahidi kwa nyakati tofauti kutoka kwa wasamaria wema, akitoa wito kwa wananchi kuendelea kuwapa ushirikiano ili kuvikomesha vitendo hivyo alivyovifananisha na uhalifu.

"Tunaomba wananchi wasikubali vitendo au makubaliano yaliyo kinyume na utaratibu kati yao na wakusanya ushuru hao kuhusu ulipaji wa ada za maegesho," anasisitiza Mkinga.

**WAHUSIKA WATHIBITISHA**

Mkurugenzi wa Kampuni ya Uwakala ya Asceric Limited inayofanya kazi ya kukusanya ushuru wa ada za maegesho ya (TATURA), Mathayo Nungu, anathibitisha kuwapo kwa baadhi ya wafanyakazi wao wanaokusanya ushuru kujihusisha na vitendo hivyo vya udanganyifu.

"Ni kweli kuna vitendo hivi na tuna wafanyakazi zaidi ya 400 ndiyo maana kuna hii changamoto, si wote wanaweza kuwa waaminifu, tayari wameshafukuzwa kazi zaidi ya wakusanya ushuru 10 baada ya kuthibitika kukiuka utaratibu wa kazi," anasema Nungu.

Kwa upande wake Ibrahim Said, mtoa huduma ya kutoza ushuru katika maegesho ya magari yaliyoko Mwenge mkoani Dar es Salaam, anakiri kuwapo tuhuma hizo dhidi yao, akisema yao wameshasimamishwa kazi.

"Wanaojihusisha na vitendo hivyo ni baadhi wasiokuwa waaminifu ambao wanaingiwa na tamaa, pasipo kufikiria kuwa wakibainika wataingia matatizo na kuharibu kazi zao. Kama bado kuna ambao wanajihusisha na vitendo hivyo nawasihi waache kwani vinatia doa utendaji wetu," anashauri Said.



## HABARI DODOMA

## 'Tuombe kumpata Spika mwaminifu'

**Peter Mkwavila,** DODOMA

WATANZANIA wametakiwa kumwomba Mungu wakati huu wa kinyang'anyiro cha kumpata Spika wa Bunge atakayewatumikia watu bila kujali itikadi ya chama chochote cha kisiasa, udini, ukabila.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Tanzania Methodist, Joseph Bundala, alitoa rai hiyo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mchakato wa kumpata Spika wa Bunge.

Alisema Watanzania wanatakiwa kuendelea kumwomba Mungu ili atupatie Spika atakayekuwa hafungamani na itikadi yoyote ile na atakayeongoza bunge kwa mujibu wa sheria.

Askofu huyo alisema wakati Watanzania wenye sifa ya kugombea nafasi hiyo muhimu ya Spika wa Bunge wakijitokeza kugombea, taifa linatakiwa kuomba ili mhimili huo kupata kiongozi atakayekuwa mwaminifu wa kuwatumikia watu na kupitisha sheria kwa mujibu wa katiba ya nchi.

"Watanzania ni muhimu wakumbuke kuwa mhimili huo ni lazima uombewe mbele za Mungu ili sheria zitakazopitishwa zikubaliwe kwa maslahi ya Watanzania na si kwa chama kimoja," alisema.

Askofu huyo aliwataka viongozi wanaochaguliwa kusimamia haki kwa ajili ya Watanzania kufanikisha maendeleo wawe waaminifu kwenye nafasi zao hizo kama walivyoaminiwa.

Alisema viongozi hao wakumbuke kuwa wamekuwa wakiapa viapo vya uaminifu na kutii mbele ya Mungu na Rais, hivyo ni lazima wawatumikie Watanzania wote bila kujali itikadi zao pamoja na serikali.

Kuhusu mabadiliko yaliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan katika Baraza la Mawaziri, alisema viongozi wanapochaguliwa wameaminiwa na serikali pamoja na Watanzania, hivyo wanatakiwa kusimamia haki kwa malengo ya kuliletea taifa maendeleo.

Licha ya maombi ya kumpata spika, aliwataka Watanzania kuomba kwa ajili ya mvua ambayo kwa mwaka huu imechelewa kunyesha kwa baadhi ya mikoa na kusababisha hofu ya baa la njaa.

**"Watanzania ni muhimu wakumbuke kuwa mhimili huo ni lazima uombewe mbele za Mungu ili sheria zitakazopitishwa zikubaliwe kwa maslahi ya Watanzania na si kwa chama kimoja," alisema.**

# RC Mtaka akerwa kiwango duni ujenzi wa madarasa

**Na Paul Mabeja,** KONDOA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, amesema hajaridhishwa na ujenzi wa madarasa yaliyojengwa na Halmashauri ya Mji wa Kondoa kutokana na kujengwa chini ya kiwango,

Mtaka alibainisha hayo juzi wakati wa kikao cha kazi pamoja na watumishi wa halmashauri hiyo.

Alisema madarasa hayo ambayo yalikuwa yajengwe ndani ya siku 90 yamejengwa na siku za nyongeza na kwa kiwango cha chini.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka viongozi wa halmashauri hiyo kuwa na ushirikano na kuacha migogoro inayosababisha kurudisha nyuma maendeleo.

"Nawapongeza kwa kumaliza ujenzi wa madarasa kwa hela mliyopewa na kumaliza kujenga madarasa hayo 24. Lakini sijaridhishwa na ujezi wa madarasa hayo. Licha ya kutomaliza kwa wakati na kupewa siku za nyongeza mmejenga chini ya kiwango," alisema Mkata.

Alisema badala ya kuendelea kuendekeza migogoro isiyo na tija, watumishi wa halmashauri hiyo watengeneze hoja zitakazoleta maendeleo kama vile kuboresha sekta ya elimu na uchumi na kuleta ushindani.

"Kondoa inaonekana mnapenda sana migogoro kitu kinachofanya kurudisha nyuma maendeleo ya halmashuri hii. Ni vyema mkatumia muda wenu kutoa hoja za kimaendeleo katika elimu na mapato namna gani ya kushindana na halmashauri zingine na ikizingatiwa nyie mna katana tu," alisema.

Viongozi wa halmashauri hiyo waliomba kuongezewe gari la taka kutokana na mahitaji kuwa mengi na gari ni moja huku idadi ya watu ikiendelea kuongezeka kila siku.

Mmoja wa viongozi hao, Mwenyekiti wa Kata ya Chimichimi alisema kata yake imekuwa na kiwango kikubwa cha uzalishaji taka kutokana na kutokuwapo kwa magari ya kutosha kuzoa taka.

Pia mkurugenzi wa halmashauri hiyo kukutana na wenyeviti wa halmashauri ili kubaini matatizo yao kwa kuwa toka ateuliwe, hajawahi kukutana nao.

"Kata yangu ya Chimchim imekuwa kama jalala kutokana na kuwa nyingi na hii inasababishwa kuwa na gari moja la taka kwa hiyo inabidi kuongezwa. Pia mkurugenzi tokea umefika katika halmashauri yetu, hujawahi kukutana na sisi wenyeviti kwa hiyo inabidi ukutane na sisi ili kujua changamoto zetu," alisema.



Katibu Msaidizi Mkuu Idara ya Oganaizesheni katika Ofisi ya Makao Makuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Solomoni Itunda (kulia), akikabidhi fomu ya kuomba kuteuliwa kugombea nafasi ya uspika wa Bunge kupitia CCM kwa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Kilolo Asia Abdallah, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# TLP yashauri serikali watoto wa mitaani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha TLP Mkoa wa Dodoma kimeishauri serikali kuweka mkazo katika kusaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi ili kuwawezesha kupata haki zao msingi zikiwamo elimu na afya.

Katibu wa chama hicho mkoa wa Dodoma, Damal Richard, alisema hayo jana jijini hapa wakati wa kutoa msaada wa vitu mbalimbali kwa kinamama na watoto waliolazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

Damal alisema serikali inatakiwa kuweka mikakati ya kusaidia watoto walio katika mazingira hatarishi ambao wamekuwa wakizagaa mitaani bila kuwa na shughuli za msingi na kupoteza haki yao za kwenda shuleni.

"Naomba serikali iweke mkazo katika kuwaondoa watoto wa mitaani ili waende kupata haki zao za msingi katika familia zao zikiwamo elimu, malazi na matibabu kama ilivyo kwa watoto wengine," alisema Richard.

Pia alisema watoto wengi wanaozurura mitaani wanazo familia zao, hivyo jamii inatakiwa kuwa mstari wa mbele katika kuwalinda.

Kiongozi huyo aliwataka kinamama kuangalia familia zao kutokana na wengi wao kuwa na shughuli za kutafuta maisha ambazo zimesababisha watoto kupotea kimaadili.

Kadhalika, alitoa wito kwa wazazi kuacha tabia ya kutelekeza watoto wanapozaliwa kwa kuwa ni kufanya hivyo ni kosa kisheria na kinyume cha maelekezo ya dini.

"Kinamama wanatakiwa kuwa na hofu ya Mungu kuacha tabia hii ya kutupa pamoja na kutelekeza watoto na kutokomea kusikojulikana," alisisitiza.

Katibu huyo alisema lengo la kutoa msaada huo ni kuwafariji kinamama hao pamoja na watoto wao ambao wamelazwa katika hospitali hiyo.

"Lakini hii kwetu ni kama kusherehekea Mwaka Mpya na wao kwa kuwapatia faraja na matumaini wakati huu wakiwa wamelezwa hospitalini ili na wao wajione kuwa pamoja na kuumwa lakini bado ni sehemu ya jamii," alisema.

Mwenyekiti wa chama hicho mkoa, Justous Silungwe, alisema viongozi wa vyama vya siasa pia wanaowajibu wa kufanya kazi za kijamii.

"Badala ya kuendelea na siasa tu pia yako majukumu mengine mengi ambayo sisi viongozi wa vyama vya siasa tunatakiwa kuyafanya katika jamii zetu nayo ni kama haya ya kutembelea wagonjwa na kauwafariji na kuona changomoto zao," alisema.

Muuguzi Mkunga wodi ya kinamama na watoto hopitali hiyo, Eveline Katabazi, akitoa shukrani kwa niaba ya uongozi, alisema msaada huo umekuja wakati mwafaka.

"Nashukuru sana kwa niaba ya uongozi wa hospitali, naomba tuendelee kushirikiana kwani Watanzania tukiwa pamoja tutafanikiwa katika changamoto mbalimbali zinazotukabili," alisema.



# Askari JWTZ mbaroni kwa tuhuma kumuua baba mzazi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linamshikilia askari wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania (JWTZ) Kikosi cha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Ruvu, mkoani Pwani, Mussa Ndonde (31) kwa tuhuma za kumuua baba yake mzazi, Edward Ndonde (75), Mkazi wa Lumbila jijini Mbeya.

Mussa anadaiwa kumcharanga baba yake kwa kisu sehemu mbalimbali za mwili wake na kisha kukata kiganja cha mkono wake.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Christina Musyani, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 3:00 asubuhi katika Mtaa wa Lumbila. Mtuhumiwa anadaiwa kufanya mauaji hayo baada ya kuingia ndani na kuchukua kisu kisha kumcharanga na kumkata kiganja cha mkono.

Kamanda Musyani alisema chanzo cha tukio kinadaiwa ni tuhuma za ushirikina kwamba Mussa alikuwa akimtuhumu baba yake kwamba ni mchawi anamloga ili asifanikiwe kwenye mambo yake.

"Awali mtuhumiwa alifika nyumbani kwa baba yake majira ya saa 3:00 pasipo kutoa taarifa yoyote ya kuja Mbeya na kuingia moja kwa moja sebuleni na kuanza kumshambulia kwa kisu na stuli na kusababisha kifo chake," alisema Musyani.

Kamanda Musyani alisema mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya kwa uchunguzi wa kitabibu huku mtuhumiwa akiendelea kupatiwa matibabu chini ya ulinzi katika hospitali hiyo baada kushambuliwa na wananchi waliojichukulia sheria mkononi kutokana na tukio alilofanya.

Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya limesema linalaani tukio hilo la kinyama kutokea na kwamba litahakikisha mtuhumiwa anafikishwa kwenye vyombo vya kisheria kwa hatua zaidi.

Pia jeshi hilo limewataka wananchi kuachana na imani potofu za kishirikina hasa kuamini waganga wapiga ramli chonganishi kwa kuwa ni hatari.

## Mbeya yabuni ujenzi shule wenye ulemavu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI ya Mkoa wa Mbeya, inakusudia kujenga shule maalum mbili za msingi na sekondari kwa watu wenye ulemavu ili kukabiliana na idadi kubwa ya watoto wanaosoma pamoja na mazingira yenye utulivu.

Hayo yalisemwa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, wakati wa kikao cha kujadili masuala mbalimbali yanayowakabili watu wenye ulemavu mkoani hapa.

Alisema wanakusudia kujenga shule za kisasa kwa watoto wenye ulemavu ambazo zitakuwa na miundombinu rafiki ya kujisomea ili kutimiza malengo yao.

Shule hizo, alisema zitakuwa za mfano nchini na kwamba serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali watakamilisha ujenzi huo.

"Tumeona vikwazo mbalimbali wanavyokabiliana navyo watoto wenye ulemavu ikiwamo madarasa na miundombinu mingine ya kujisomea watoto hao. Sasa ujenzi wa shule mbili za msingi na sekondari utakuwa mwarobaini wa kutatua shida hiyo," alisema.

Ofisa Taaluma Mkoa wa Mbeya, Wilbroad Yanga, alisema serikali imetoa Sh. bilioni 15 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Alisema shule ya msingi yenye mahitaji maalumu ya Katumba II iliyoko wilayani Rungwe, imetengewe Sh. milioni 80 kwa ajili ya ujenzi wa bweni, Sh. milioni 90 ujenzi wa jengo la utawala na vyumba vitatu vya madarasa lengo likiwa ni kupunguza msongamano wa watoto shuleni hapo.

Alisema Shule ya Msingi Katumba II inakabiliwa na tatizo kubwa la miundombinu ya madarasa kutokana na mrundikano wa wanafunzi ambao wanatoka maeneo mbalimbali nchini.



Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vicent Anney (wapili kulia), akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, meza na kiti kama ishara ya kukabidhi madarasa 74 ya wilaya hiyo, mkoani humo juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# RC awabana ma-DC, ma-DED uandikishaji wanafunzi

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameziagiza wilaya na halmashauri zote za mkoa kila ifikapo Ijumaa kupeleka ripoti ya wanafunzi wa darasa la awali walioandikishwa katika shule mbalimbali za msingi.

Homera alitoa agizo hilo juzi alipofanya ziara kukagua miradi mbalimbali inayotekelezwa na serikali kupitia fedha za UVIKO-19 katika sekta za afya na elimu katika Wilaya ya Rungwe na Halmashauri ya Busokelo.

Alisema ripoti za idadi ya watoto walioandikishwa katika madarasa awali zinapaswa kuanza baada ya shule kufunguliwa.

"Licha ya mkoa wetu kuwa miongoni mwa mikoa iliyojitahidi kuandikisha wanafunzi wa darasa la awali nchini kwa wastani wa asilimia 46, hali hairidhishi. Tuongeze kasi ya kuwaandikisha watoto wetu waliofikia umri wa kuanzia miaka minne ili tuendelee kufanya vizuri kitaifa na pia wanafunzi wetu kupata elimu kwa wakati mwafaka," alisema Homera.

Katika hatua nyingine, Homera alikabidhiwa zaidi ya vyumba vya madarasa 70 ambavyo ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 100 kwa ajili ya kutumiwa na wanafunzi wa kidato cha kwanza.

Aliwapongeza viongozi wa Wilaya ya Rungwe pamoja na Halmashauri ya Busokelo kwa kukamilisha kwa wakati vyumba vya madarasa. Sambamba na hilo walijenga shule mpya za sekondari kupitia fedha hizo walizopewa kujenga vyumba vya madarasa.

"Nawapongeza sana viongozi kwa ubunifu huu wa kujenga shule mpya za sekondari sita mliona kuliko kuongeza vyumba vya madarasa sehemu moja ni afadhali mkaanzisha shule mpya za sekondari kwenye kata ambazo hazikuwa nazo ili kuwarahisishia watoto wetu kupata elimu," alisema Homera.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Mpokigwa Mwankuga, aliishukuru serikali kwa kuwapatia fedha nyingi kwa ajili ya kujenga miradi mbalimbali ya maendeleo na kwamba imewarahisishia wananchi kupata huduma za kijamii karibu na makazi.

Aliongeza kuwa licha ya kukamilika kwa miradi hiyo ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya, zahanati na shule bado kuna tatizo kubwa la uhaba wa watumishi, aliiomba serikali kuajiri watumishi hao ili wananchi kupata huduma za kijamii ikiwamo matibabu na elimu kwa wakati.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vicent Anney, alisema miradi yote inayoendelea kutekelezwa na serikali inasimamiwa kikamilifu kwa kushirikiana na wananchi.

Alisema anatamani miradi yote ya afya ikamilike ifikapo Aprili, mwaka huu, ili wananchi katika maeneo yao waanze kupata huduma za matibabu na kuwapunguzia gharama ya kusafiri umbali mrefu.



# Mahitaji ya mkaa yaathiri hekta 470,000 za ardhi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

HEKTA 470,000 za ardhi zenye misitu zinaathiriwa nchini Tanzania kwa mwaka kutokana na ukataji miti kwa ajili ya nishati ya mkaa.

Hayo yalisemwa jana na Mhandisi wa Migodi wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Charles Mawala, wakati akitoa mada ya matumizi ya mkaa mbadala katika kongamano la utunzaji wa mazingira lililofanyika viwanja vya Maisara mjini Zanzibar.

Alisema hali hiyo inaathiri mazingira kwa sababu miti husaidia kuvuta hewa chafu kama carbodioxide inayotokana na shughuli zote za kibinadamu.

"Gesi hizi huchangia pakubwa kwenye uharibifu wa tabaka la ozone na kusababisha majanga kama ukame," alisema.

Alisema kutokana na ongezeko hilo la ukataji wa miti kila mwaka, STAMICO iko mbioni kuanza uzalishaji wa mkaa mbadala (rafiki briquettes) ambao ni mwafaka kwa matumizi ya kijamii. Mawala alisema mkaa huo ni suluhisho kwa tatizo la kimazingira la hatari ya kutokea jangwa inayosababishwa na ukataji ovyo wa misitu kwa ajili ya nishati ya kuni na mkaa wa kuchoma.

"Rafiki briquettes ni mkaa unaozalishwa kutokana na makinikia ya makaa ya mawe yanayochimbwa kwenye mgodi wa Kiwira, mkoani Mbeya," alisema.

STAMICO, alisema imekusudia kusaidia Watanzania kuwa na nishati mbadala ya kudumu na yenye ufanisi mkubwa na tayari mitambo miwili yenye uwezo wa kuzalisha tani ishirini kwa saa sio kwenye mchakato wa ununuzi.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, Sheha Mjaja Juma, alisema kutokuwapo kwa mpango wa matumizi ya ardhi kunaongeza kasi ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira.

Alisema kwa mujibu wa ripoti za awali za uchambuzi wa hali halisi ya mfumo wa usimamizi wa taka ya mwaka 2018, kwa wastani Zanzibar inazalisha tani 238,713 za taka kwa mwaka ambapo ni sawa na tani 654 kwa siku.

"Wastani wa asilimia 80 ya taka zinatolewa Zanzibar ni taka zinazooza (organic). Hii inaashiriwa kuwa taka hizo zinaweza kutumika kusaidia kuimarisha kilimo kama zinatengenezwa mbolea," alisema.

Pia alisema wastani wa asilimia 40 ya taka zinazotolewa kila siku Zanzibar ndizo huchukuliwa na kutupwa katika maeneo rasmi yaliyopangwa na asilimia 60 ya kiwango cha taka kinachotolewa kwa siku hutupwa ovyo kwenye maeneo yasiyo rasmi na kuwa tishio kwa afya ya jamii na mazingira.

Alisema kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia mwaka 2018, Zanzibar inatoa kilo 378,211 za taka hatari zinazotokana na matibabu hospitalini kwa mwaka sawa na wastani wa tani moja kwa siku.

Alisema wastani wa mifuko ya uzazi (placentas) 42,546 kwa mwaka inatolewa, mfuko 3,546 kwa mwezi na 118 kwa siku na hakuna mfumo mzuri wa kusimamia ipasavyo taka za aina hiyo.

Akifunga mafunzo hayo Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO, Dk. Venance Mwasse, alisema kuna umuhimu wa utunzaji wa mazingira kwa ajili ya maslahi ya vizazi vya sasa na baadaye.

Alisema kuna fursa nyingi za vijana katika taka ikiwamo ajira katika kujenga uchumi wao na nchi, lakini taka ni malighafi na chanzo cha viwanda na uzalishaji wa pato la taifa.




Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Dk. Venance Mwasse, akizungumza katika kongamano la utunzaji wa mazingira, katika viwanja vya Maisara, Mjini Zanzibar jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRED), Latifa Khamis. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Filamu ya Samia kuzinduliwa Aprili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

FILAMU maalumu iliyojulikana kwa jina la "The Royal Tour" ambayo imewashirikisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, inatarajiwa kuzinduliwa Aprili, mwaka huu, nchini Marekani.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Muhammed Mussa, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya wizara hiyo.

Alisema kukamilika kwa filamu hiyo kutaitangaza vyema Tanzania katika nyaja za uwekezaji, utalii na uhusiano wa kidiplomasia.

Pia alisema wizara yake inaendelea na jitihada za kuitangaza vyema Zanzibar kitaifa, kikanda na kimataifa katika sekta ya utalii.

Waziri huyo alisema kazi hiyo imesababisha kuongezeka kwa wageni wanaoingia nchini. Alisema wageni 310,580 wameingia kwa kipindi cha Januari hadi Oktoba, mwaka jana ikilinganishwa na mwaka 2020 walikuwa 260,644. Idadi hiyo ni ongezeko la wageni 49,936 sawa na asilimia 84.

Alisema wizara inaendelea kushirikiana na wadau wa sekta ya utalii katika utaratibu wa kuandaa na kubuni shughuli tofauti zitakazopelekea kuongeza siku za ukaazi kwa wageni wanaoingia nchini.

"Katika kulifanikisha hili, wizara imeshiriki matamasha manane ya kitaifa, kikanda na kimataifa yakiwamo East Africa Tourism Expo, Sun Wave, Sea Food Festival. Kufanyika kwa matamasha haya, kunaongeza siku za ukaazi kwa wageni pamoja na idadi ya watalii wanaotembelea nchini," alisema.

Pia alisema wizara yake imefanikiwa kuwatumia watu maarufu duniani wakiwamo wachezaji wa mpira na waigizaji wa filamu za kimataifa ambao wamefika Zanzibar na kushirikiana nao katika kuitangaza Zanzibar.

Alisema miongoni mwa watu maarufu hao ni mchezaji wa Leicester City FC, Mamadou Sakho, mchezaji wa kimataifa wa Argentina anayechezea klabu PSG ya Ufaransa, Mauro Icardi, na mwigizaji maarufu kutoka India, Sanjidati.

"Ni wazi kwamba watu hawa niliowataja ni maarufu sana duniani kote, hivyo kuwatumia katika kuitangaza Zanzibar ni kuongeza idadi ya wageni wanotarajiwa kufika nchini mwetu kutoka mataifa tofauti," alisema.

## Waziri asisitiza utoaji risiti EFD

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Jamal Kassim Ali, amewataka, wananchi kujenga utaratibu wa kudai risiti wanaponunua bidhaa na wafanyabiashara kutoa risiti wanapofanya mauzo.

Jamal alisema, sheria imeelekeza kwamba kutokutoa risiti ni kosa kwa mujibu wa sheria ambapo kosa hilo adhabu yake ni kifungo cha miezi sita hadi mwaka mmoja au faini ya shilingi milioni 2 hivyo, aliwataka wafanyabiashara kufuata sheria bila shuruti.

Waziri alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya ziara yake ya siku moja kisiwani Pemba ya kuzungumza na wafanyabiashara wa maduka na hoteli.

Alisema moja ya mambo ambayo serikali inatilia mkazo katika kipindi hiki ni utoaji wa risiti katika maduka, hivyo serikali kupitia Bodi ya Mapato Zanzibar imetengeneza mfumo ambao unatoa risiti za kielektroniki.

Jamal alisema risiti hizo zitarahisisha utendaji wa biashara ndani ya nchi na kusaidia upatikanaji wa mapato ya serikali na kupunguza upotevu wa mapato. Alisema kupitia kikao hicho, ameona kuna haja ya kupita kwa wafanyabiashara kuona namna ambavyo wanatumia mashine hizo.

"Tumejionea na kuna baadhi ya changamoto na kuna haja ya kuzitatua ikiwamo baadhi ya wafanyabiashara kutojua kuzitumia mashine. Kuna haja ya kutoa mafunzo na pia kuna tatizo la mawasiliano, tulipopita hotelini wamesema mtandao unakuwa chini kwa hivyo hawawezi kuutumia mfumo huo," alisema.

Alisema lengo la ziara hiyo ni mwendelezo wa kikao chake alichokifanya na wafanyabiashara wa Pemba kujadiliana changamoto, mipango na masuala mbalimbali ya kuhakikisha wanafanya biashara zao kwa ufanisi.

Nao wafanyabiashara hao walisema utaratibu wa mashine za kielektroniki wameupokea vizuri licha ya kuwa kunahitajika elimu zaidi juu ya suala hilo lakini kwa hatua za mwanzo wanaendelea vizuri.

Juma Ali, mmoja wa wafanyabiashara hao, alisema changamoto ndogo zimekuwa zikijitokeza ikiwamo kupotea mawasiliano na baadhi ya mashine zinatoa kiwango cha pesa ambacho sicho, ni tofauti na ambazo zinatoka kwenye risiti na wanazoziandika wao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

COMPANY NO: 120197

**SPECIAL RESOLUTION**

**EXTRACT FROM THE MINUTES IF THE MEMBERS MEETING OF THE SHARAHOLDERS OF THE COMPANY HELD AT REGISTERED OFFICE, MABUTO FOOD PRODUCTION COMPANY HEAD OFFICE ON THE 04TH JANUARY 2022.**

**MABUTO FOOD PRODUCTION COMPANY LIMITED**

Upon a motion duty made, seconded and unanimously carried on 04th Jan 2022 by the board of members

It was **RESOLVED** to wind up the Company voluntarily in accordance will section 333(1) of the companies Act No, 12 of 2002.

It was **FURTHER RESOLVED THAT**; the Company confirm that there is no reason to prevent the dissolution of the Company.

It was **FURTHER RESOLVED THAT**; SAB Attorneys has been appointed as the liquidator for the purpose of winding up of the Company.

The meeting was successfully called off and the minutes signed accordingly on 04th Jan 2022

Signature ……………………
**PASTORY CHARLES MABUTO**
Chairman

Signature ……………………
**DANIEL LUSHONA MIGEKA**
Secretary

## KUPOTEA KWA VYETI



ATHUMAN MOHAMED anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye index namba S.1261/0046 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya MERRIWA mwaka 2004 na cheti cha chuo BUSTANI TEACHER'S COLLEGE kozi ya UALIMU GRADE A chenye namba E.511/0128 mwaka 2006,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa DOD/DOD/RB/12979/2022

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

SIMON SALATIEL SHEMHILU anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA CROWN yenye namba za usajili T 542 DPU chasis namba GRS1800001620,engine namba 4GREAA1620,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa DAR/URA/RB/18373/2022

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 73 OF 2021**

**In the Matter of the Estate of the Late GEORGIES FRANK MGODE**

**BY 1. ANNASTAZIA NDOROBO MBISE**
**2. ……………………………….**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 25 day of JAN….2022
**Dated at Morogoro this 05 day of JAN…..2022**

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 203 of 2021**
**In the matter of the Estate of the late of the late CHALE KAJURA MAGAMBO of Kilimani within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by REGINA MELKIORY TAWA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 14 day of 2,2022
**Dated at Dodoma this 11 day of 1, 2022**

RESIDENT MAGISTRATE

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF MALINYI**
**AT MALINYI**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 01 of 2021**
**In the matter of the Estate of the late LUTGER DAUD CHIPINDI**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by SINGLINDA ALFRED CHIWALANGA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above - named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 18 day of 01,2022
**Dated at MALINYI this 10 day of 01, 2022**

*Registrar/senior resident magistrate*
RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
P.O. BOX ….MALINYI

**IN THE COURT OF DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 169 of 2021**
**In the matter of the estate of the late of the late ENZI JORAM ELIASI of Majengo Area within**
**Dodoma Regional**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by TELESIA BRAZIO FATAKI**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 13 day of Jan,2022
**Dated at Dodoma this 20 day of 12, 2021.**

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 206 of 2021**
**In the matter of the Estate of the late CHRISTOPHER ORGENES CHIWAMBA of IMAGE**
**Within Dodoma Region.**
**And**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY BLANDINA BENJAMIN CHIWAMBA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 163)**

All PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 27 day of January,2022
**Dated at Dodoma this 30th day of DECEMBER 2021**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

ATHUMANI SAIDI PEMBE anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki aina ya BOXER yenye namba za usajili MC 548 CVZ. yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi.
DOD/MPW/RB/13577/2022.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA:Taraka 40….2021**
**MDAI: DIANA JAFARI**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: EPHATI SWAI**
**Kwa: EPHATI SWAI**
**Ombi la mdai: DIANA JAFARI**
**Madai ya :Mgawanyo wa mali**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikiliwa mnamo **tarehe 01 mwezi 02 mwaka 2022 saa8:30 asubuhi.**
Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama itathibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa Shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo **tarehe 07 mwezi 01 mwaka 2022.**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mhadhiri jela rushwa ya ngono, akihonga mitihani

**Rabat,** MOROCCO

PROFESA wa Chuo Kikuu cha Morocco, anayeshutumiwa kwa kuwapa wanafunzi alama nzuri kama malipo ya upendeleo wa ngono amefungwa jela kwa miaka miwili.

Ni hukumu ya kwanza katika msururu wa kesi za unyanyasaji wa kijinsia maarufu katika vyuo vikuu, Morocco.

Mhadhiri huyo wa masuala ya uchumi katika Chuo Kikuu cha Hassan I, karibu na Casablanca, alipatikana na hatia ya tabia chafu miongoni mwa mashtaka mengine.

Wasomi wengine wanne, walitarajiwa kufikishwa mahakamani siku ya jana kama sehemu ya kashfa hiyo.

Kesi hizo ziliangaziwa na vyombo vya habari vya Morocco mwaka jana, baada ya wanahabari kuchukua ujumbe tofauti ulioripotiwa, kati ya wanafunzi na wahadhiri.

Wanaharakati wanasema ni nadra kwa kesi za unyanyasaji wa kijinsia kufikishwa mahakamani.

**BBC**



Wanajeshi wa Lebanon wakiwa katika jaribio la kufungua barabara iliyofungwa na madereva wakati wa maandamano ya kupinga kupanda kwa bei ya petroli na hali mbaya ya kiuchumi, mjini Sidon, jana. **PICHA: REUTERS**

## Nigeria yafuta marufuku ya Twitter baada ya miezi saba

**Lagos,** NIGERIA

NIGERIA imeondoa marufuku yake dhidi ya Twitter, miezi saba baada ya kubana matumizi ya mtandao huo wa kijamii.

Serikali ya Nigeria ilisimamisha Twitter Juni mwaka jana, baada ya kampuni hiyo kufuta ujumbe wa Twitter wa Rais Muhammadu Buhari, kuhusu kuwaadhibu wanaotaka kujitenga nchini humo.

Mamlaka zilishutumu kampuni hiyo ya mitandao ya kijamii kwa kuegemea upande wa watu wanaotaka kujitenga.

Serikali ilisema inabadilisha marufuku hiyo baada ya Twitter kukubaliana na masharti, ikiwa ni pamoja na kufungua ofisi ya ndani, Nigeria.

Hatua hiyo inaruhusu mamilioni ya watu katika taifa hilo lenye watu wengi zaidi barani Afrika, kutumia mtandao huo tena.

Baadhi ya watumiaji walikuwa wameendelea kufikia tovuti hiyo, baada ya kusimamishwa kwa kutumia mitandao ya kibinafsi (VPNs), serikali iliapa kuwabana wale ambao bado wanatuma ujumbe kwenye Twitter, ikiwa ni pamoja na mashirika ya vyombo vya habari.

Hatua ya mwaka jana ya serikali ya Nigeria, ilizua malalamiko ya kimataifa kuhusu uhuru wa kujieleza.

Uamuzi wa kampuni hiyo ya mitandao ya kijamii kujiandikisha nchini humo, ulionyesha kujitolea kwa Nigeria, shirika la maendeleo ya teknolojia ya habari, lilisema.

Twitter bado haijatoa maoni yoyote kuhusu uamuzi wa Nigeria wa kuondoa marufuku hiyo.

Serikali iliamuru watoa huduma za mtandao kuzuia Twitter, kwa madai kuwa ilikuwa inatumiwa kudhoofisha uwepo wa Nigeria, kama nchi kupitia kueneza habari za uongo ambazo zinaweza kuwa na madhara ya vurugu.

Baada ya Twitter kuondoa chapisho la Rais Buhari lililorejelea vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Nigeria vya mwaka 1967 hadi 1970 na kuwachukulia wale wanaofanya vitendo vibaya, kama wasioitakia mema nchi hiyo.

Twitter ilisema ni maarufu kwa Wanigeria wengi na jukwaa hilo limetumika kama zana ya kuhamasisha.

Wanaharakati waliitumia kutafuta uungwaji mkono wakati wa maandamano dhidi ya ukatili wa polisi, chini ya alama ya #EndSars, ambayo ilivutia watu duniani kote.

**BBC**

## ECOWAS yaleta msukosuko kisiasa Ivory Coast

**Abidjan,** IVORY COAST

VIKWAZO vilivyowekwa na Jumuiya ya Kiuchumi ya Mataifa ya Afrika Magharibi (ECOWAS), dhidi ya utawala wa Mali, vimesababisha msukosuko wa kisiasa nchini Ivory Coast.

Saa chache baada ya kutangazwa kwa vikwazo hivyo, baada ya kuandamana na kuwaita mabalozi wake katika eneo hilo, Mali ilimwachilia huru balozi wa zamani wa Soroist, ambaye aliombwa na mahakama ya Ulaya kumrejesha nyumbani.

Hata hivyo, Chama cha Laurent Gbagbo, kimejitokeza na kushutumu vikwazo hivyo.

Chama kipya cha Pan-Africanist cha Laurent Gbagbo kinaona hatua za kulipiza kisasi zilizochukuliwa na ECOWAS dhidi ya raia wa Mali, kuwa ni nyingi na zisizofaa.

Katika taarifa iliyotiwa saini na msemaji wake, Justin Kone Katinan, PPA-CI pia amekitaja kile alichokiita kutokubalika na hatari kwa kile anachokichukulia kama kutumiwa kwa taasisi za fedha na benki za jumuiya kutatua masuala ya ndani ya kisiasa.

Ishara kwamba uhusiano ulidorora Jumapili jioni, kati ya Mali na majirani zake, utawala wa kijeshi wa nchi hiyo uliwaita nyumbani mabalozi wake katika ukanda huo.

Na siku ya Jumatatu mjini Bamako, mbunge wa zamani anayemuunga mkono Soro, Sess Soukou Mohamed, anayejulikana kwa jina la Ben Souk, aliachiliwa ghafla, usiku wa kuamkia siku yake ya kusikilizwa na jaji.

Ben Souk, alikamatwa Agosti 10 na kusafirishwa kwenda Ivory Coast.

Ben Souk, pia alihukumiwa kifungo cha miaka 20 bila kuwapo mahakamani, Juni mwaka huu, kwa kuhatarisha usalama wa mamlaka ya serikali na kula njama.

Kesi ambayo ilimfanya Guillaume Soro, ahukumiwe bila kuwapo kwa kifungo cha maisha.

Guillaume Soro, alikaribisha kuachiliwa kwa mshirika wake wa kisiasa katika taarifa ambayo alionyesha uungwaji wake mkono wa dhati kwa mamlaka ya mpito, bila hata kutoa maoni yake kuhusu vikwazo.

Mtu mwingine maarufu ambaye alighadhabishwa na vikwazo vya ECOWAS, ni mwanamuziki nguli wa mitindo ya Reggae, Alpha Blondy.

**RFI**

## Ujerumani yamhukumu maisha ofisa wa kijasusi

**Koblenz,** UJERUMANI

MAHAKAMA ya Ujerumani, imemhukumu kifungo cha maisha jela, ofisa wa zamani wa kijasusi, aliyehudumu idara za kijasusi za serikali ya rais Bashar al Assad katika kesi ya kihistoria ya uhalifu dhidi ya ubinadamu katika vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Anwar R amekutwa na hatia ya makosa 58, yaliyomkabili yakiwamo mauaji, ubakaji na unyanyasaji wa kingono kwenye gereza moja la mjini Damascus, lililokuwa likisimamiwa na idara ya kijasusi iliyokuwa chini yake.

Hukumu hiyo ni ya pili kutolewa na mahakama ya juu iliyoko katika mji wa Koblenz katika mashtaka hayo ya uhalifu dhidi ya ubinadamu katika mzozo.

Mwaka jana, Eyad A mtumishi wa zamani wa idara za kijasusi, Syria, alihukumuiwa kifungo cha miaka minne na nusu gerezani kwa madai ya kusaidia mateso dhidi ya raia.

**DW**

# MSHERY AELEZEA LADHA YA KUDAKIA YANGA SC

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA mpya wa Yanga, Aboutwalib Mshery aliyesajiliwa kipindi cha dirisha dogo akitokea Mtibwa Sugar ameeleza tofauti ya kudakia timu hizo mbili kuwa ni wingi wa mashabiki ambao wamekuwa wanamwangalia, kumshangilia na kumpa sapoti kiasi cha kujikuta anajituma zaidi.

Mshery ambaye aliidakia Yanga kwa mara ya kwanza Desemba 31, mwaka jana, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kati ya timu yake hiyo mpya dhidi ya Dodoma Jiji na kutoruhusu bao, Yanga ikishinda mabao 4-0.

Alisema kuwa, pamoja na kwamba Mtibwa Sugar ilikuwa na mashabiki ambao walikuwa wanampa sapoti, lakini kuna utofauti mkubwa wa kudakia timu hiyo na timu kubwa kama Yanga.

"Kwanza nimegundua kumekuwa na mashabiki wengi wamekuwa wakinifuatilia, kuniunga mkono na kunishangilia iwe uwanjani au kwenye televisheni, hivyo inanipa ari ya kujituma zaidi kwa ajili ya kutowaangusha," alisema.

"Kwa mara kwanza nilipovaa jezi ya Yanga niliona kuna utofauti, kwani nilikuwa napewa sapoti na kushangiliwa na mashabiki wengi, hii imenipa sana morali ya kujituma zaidi," alisema.

Kuhusu kujiunga na timu ambayo ina kipa wa kimataifa kutoka Mali, Djigui Diarra ambaye anaweza kumeza kipaji chake, Mshery amesema hadhani kuna kitu kama hicho na kuongeza kuwa hata yeye mwenyewe amefurahi kukutana na kipa huyo mzoefu na kwa sababu yeye bado chipukizi anaamini kuna vitu vingi atajifunza kutoka kwake.

"Nichoshukuru ni kwamba nimekuja kukutana na kipa mzoefu na wa kimataifa, kwa hiyo kipaji nilichonacho na nikiongeza na uzoefu nitakaoupata kutoka kwake, basi nitafanya vizuri zaidi."



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi akiwa na mkewe, Mariam Mwinyi wakisalimiana na Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Tabia Maulid Mwita (kulia) na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Idrisa Mustafa Kitwana alipowasili kuhudhuria hafla ya taarabu ya kusherehekea miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar katika ukumbi wa Sheikh Idrisa Abdulwakil Kikwajuni, juzi. **PICHA: IKULU**

# Tanzanite yajipanga kuiondoa Ethiopia

**Na Saada Akida, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Wanawake, Tanzanite, Bakari Shime, amesema kazi kubwa iliyobakia ni benchi la ufundi kuandaa timu kuwa imara nyanja zote kwa ajili ya mchezo dhidi ya Ethiopia.

Tanzanite juzi iliwasili Visiwani humo kwa ajili ya kambi ya kujiandaa kwa mchezo wa raudi ya nne wa kufuzu Kombe la Dunia mwaka huu nchini Costa Rica.

Akizungumza na gazeti hili jana, Shime alisema kikosi kimewasili salama visiwani humo na wameendelea na programu ya mazoezi katika Uwanja wa Amaan, kwa ajili ya kukabiliana na wapinzani wao Ethiopia.

Alisema kiutawala kila kitu kimeenda vizuri kazi kubwa iliyobakia ni benchi la ufundi kufanya majukumu yao ya kuhakikisha wana imarisha kila sekta ili kufanya vizuri katika mchezo huo.

"Mechi hii itakuwa ngumu kwa sababu ni muhimu kwa kila upande ikiwamo kwetu pamoja na Ethiopia, tunahitaji kufanya maandalizi mazuri kwa ajili ya kutafuta matokeo chanya katika mchezo huu nyumbani," alisema.

"Ethiopia sio timu ya kuibeza, tunafanya maandalizi ya kutosha kuhakikisha tunapata ushindi mbele ya wapinzani wetu hao," alisema Shime.

Tanzanite imesonga mbele baada ya kuiondoa Burundi kwenye raundi iliyopita kwa ushindi wa jumla ya michezo miwili kwa mabao 4-3.

Mchezo wa mkondo wa kwanza uliochezwa Dar es Salaam, Tanzanite iliibuka na ushindi wa 3-2 na wamarudiano uliochezwa Desemba 18, 2021, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1.

Kwenye mchezo huo wa marudiano uliopigwa nchini Burundi Desemba 18, mwaka jana, kikosi cha Tanzania kilicheza pungufu ikiwamo wachezaji 8 tu uwanjani baada ya 11 kuripotiwa na maambukizi vya virusi vya corona.

Tanzania wanakuwa wenyeji dhidi ya Ethiopia kwenye mchezo wa raundi ya nne, utakaopigwa Januari 23, 2022, katika Uwanja wa Amaan, Zanzibar na marudiano kati ya Februari 4 hadi 6, 2022.

## Jonas Mkude alivyomshawishi Pablo kumwamini

**Na Saada Akid, Zanzibar**

KIUNGO wa Simba, Jonas Mkude, amesema siri kubwa ya kiwango kizuri ni kujituma mazoezini na kumshawishi Kocha Pablo Franco kumwamini na kumpa nafasi katika kikosi cha kwanza.

Mkude amekabidhiwa tuzo na kitita cha Sh. milioni mbili baada ya kuibuka kuwa mchezaji bora wa mashabiki wa Desemba 2021 (Emirate Aluminum Simba ACP Fans Player of the Month )2021.

Kiungo huyo alionyesha kiwango kizuri Desemba akiwashinda walinzi wa kati, Joash Onyango na Henock Inonga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkude alisema kwa sasa ndani ya kikosi chao kuna changamoto ya kupambania namba na kila mmoja anahitaji kumshawishi kocha ili kumpa nafasi.

Alisema alikaa nje muda mrefu bila kucheza, lakini hatua hiyo haikumwathiri kisaikolojia hadi kushuka kiwango zaidi ya kupambana katika mazoezi kwa lengo la kumshawishi kocha kumpa nafasi ndani ya kikosi cha kwanza.

"Changamoto ya namba ipo, kila mtu anatakiwa kujitoa na kupambania timu kufanya vizuri na kufikia malengo, kazi yangu ni mpira, kukaa nje kwa muda mrefu haikuniathiri kushuka kiwango changu," alisema Mkude.

## Messi wa Tanga atua Dodoma Jiji

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Dodoma Jiji, imekuwa moja kati ya timu iliyoibomoa Coastal Union baada ya kumsajili straika Issa Abushehe 'Messi wa Tanga' ikiwa ni siku moja tu kabla ya kufungwa na dirisha dogo la usajili.

Mtandao rasmi wa instagram wa klabu ya Dodoma Jiji umechapisha taarifa na picha ya mchezaji huyo, ukimkaribisha kwenye klabu hiyo ya 'walima zabibu' wa Dodoma.

Kuondoka kwa Abushehe kwenye klabu ya Coastal Union kunafuatia kuondoka kwa mchezaji Mudathir Said aliyejiunga na klabu ya Prisons, pamoja na Hamad Rajab 'Majimengi' ambaye ametangazwa rasmi kujiunga na Ruvu Shooting.

Hata hivyo, Katibu Mkuu wa Coastal Union, Rashid Mgweno, amesema kuwa Abushehe amekwenda Dodoma Jiji kwa mkopo na si kwamba amemsajili.

"Tumempeleka kwa mkopo kwa muda wa miezi sita. Ni mchezaji wetu ambao msimu huu ameongeza mkataba kwa mwaka mmoja, na alikuwa anamaliza kipindi hiki cha dirisha dogo mkataba wa awali, kwa hiyo ana mwaka mzima kwetu. Alikuwa hachezi kwa muda mrefu, kwa hiyo ameomba aende kwenye timu ambayo atacheza kwa miezi sita kwa sababu tuna mpango wa kumpeleka nje ya nchi akimaliza miezi sita yake," alisema Katibu Mkuu huyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### PSG WAMTAKA POGBA
PARIS St-Germain wana nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United, Paul Pogba, huku Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 28 pia akitaka kuhamia klabu hiyo ya Ligue 1. ***(L'Equipe)***

### LAMPTEY AWINDWA MAN
MANCHESTER United wanawania kumsajili mlinzi wa kulia wa Brighton, Tariq Lamptey. Brighton wanataka pauni milioni 40 kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(Mail)***

### ZAKARIA ATAKIWA UNITED
MANCHESTER United imefanya mawasiliano na kiungo wa Borussia Monchengladbach na Uswisi, Denis Zakaria mwenye umri wa miaka 25. ***(Christian Falk - Sport Bild)***

### MELO AWANIWA ARSENAL
ARSENAL wamefanya mawasiliano na Juventus kuhusu mkataba wa mkopo wa kiungo wa kati wa Brazil, Arthur Melo mwenye umri wa miaka 25. Pia wanamlenga kiungo wa kati wa Leicester na Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye miaka 24. ***(Goal)***

### ARSENAL WAKOMAA NA VLAHOVIC
KLABU ya Arsenal bado wanavutiwa na mshambuliaji wa Fiorentina, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21. ***(Sky Sports)***

### POCHETTINO ASUBIRIWA MAN
KOCHA wa PSG, Mauricio Pochettino bado anawasiliana na Manchester United kuhusu uhamisho wa majira ya joto. Kocha sasa wa muda, Ralf Rangnick anamtaka bosi wa Ajax, Erik ten Hag. ***(Le Parisien, via Sun)***

### RUDIGER KUBAKI CHELSEA
MLINZI wa Chelsea, Antonio Rudiger sasa anapanga kubakia pale Stamford Bridge. Raia huyo wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 28, ambaye mkataba wake unamalizika msimu ujao alikuwa akihusishwa na kutaka kuondoka. ***(Bild, via Teamtalk)***

### BISSOUMA ATAKIWA VILLA
KLABU ya Aston Villa inawania saini ya kiungo wa kati wa Brighton, Yves Bissouma mwenye umri wa miaka 25. ***(Telegraph)***

### BENKOVIC MKATABA BASI
LEICESTER City na mlinzi wake, Filip Benkovic wamekubaliana kusitisha mkataba wa nyota huyo wa kimataifa wa Croatia mwenye umri wa miaka 24. ***(Leicester Mercury)***

### DEMBELE KUTIMKIA MAN
UOSMANE Dembele anatazamiwa kuondoka Barcelona mwishoni mwa msimu huu na Manchester United wanamtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 24. ***(Mirror)***

### BERGWIJN AKATALIWA
KLABU ya Tottenham Hotspur imekataa ombi la winga wa Uholanzi, Steven Bergwijn mwenye umri wa miaka 24 kutoka Ajax. ***(Talksport)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# INZAGHI: WACHEZAJI INTER MILAN WATAPEWA ZAIDI

●●● Asema rais wa klabu hiyo atawapa baada ya kutwaa taji la Supercoppa Italiana na...

**MILAN, Italia**

WACHEZAJI wa Inter wanajipanga kupewa "zawadi" kutoka kwa rais wa klabu hiyo, Steven Zhang baada ya ushindi wa 2-1 kwenye fainali ya Supercoppa Italiana dhidi ya Juventus, kwa mujibu wa kocha, Simone Inzaghi.

Nerazzurri walinyanyua taji la kwanza kwa msimu huu katika soka la Italia katika muda wa nyongeza, huku Alexis Sanchez akifunga bao la ushindi.

Weston McKennie alianza kuweka mbele Juve, kabla ya Lautaro Martinez kusawazisha kwa mkwaju wa penalti, juzi Jumatano.

Timu hizo zilionekana kutoshana nguvu katika muda wa kawaida na ule wa ziada wa dakika 30, hadi makosa ya Alex Sandro yalipomruhusu Matteo Darmian kummegea pande zuri Sanchez, ambaye alifunga katika dakika ya mwisho kabisa kwenye mchezo huo na kuibua shangwe.

Hiyo imemfanya Inzaghi kuwa kocha wa kwanza kuifunga Juventus katika fainali tatu (tangu msimu wa 1929-30).

Inzaghi alizungumza kwa ufupi baada ya mchezo huo kabla ya kumpeleka msaidizi wake kwenye mkutano wa waandishi wa habari baada ya kupoteza sauti, akielezea kile ambacho rais Zhang alichowaambia wachezaji.

"Yeye (Zhang) alikuwa na furaha kubwa," alisema Inzaghi akiiambia Mediaset. "Ameileta timu pamoja na kutuhakikisha zawadi sisi.

"Wachezaji walijibu vizuri, walitaka zawadi na nafikiri rais atawapatia."

Inter imeshinda kwa mara ya sita kombe hilo ikiwa nyuma ya Juventus (mara tisa) na AC Milan (mara saba) na wamelitwaa kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2010.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 846

MECHI KALI
RUVU SHOOTING
VERSUS
MTIBWA SUGAR
1 | 2.25
X | 2.75
2 | 3.43

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ANCELOTTI ASIFIA NYOTA KUTINGA FAINALI SUPERCOPA



**RIYADH, Saud Arabia**

KOCHA Mkuu wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amesema wachezaji walikuwa wamechoka, lakini walikuwa na furaha kubwa baada ya ushindi wa 3-2 kwenye nusu fainali ya Supercopa de Espana dhidi ya Barcelona.

Los Blancos hao sasa wamefuzu kucheza fainali baada ya ushindi huo katika muda wa zaidi pale kwenye uwanja wa King Fahd nchini Saudi Arabia, Jumatano.

Madrid waliongoza mara mbili, kabla ya kwenda muda wa ziada kwa mabao ya Vinicius Junior na Karim Benzema ambayo yalisawazishwa na Luuk de Jong na Ansu Fati.

Lakini kikosi hicho cha kocha Ancelotti kilipata bao la ushindi lililofungwa na Federico Valverde aliyetokea benchi katika dakika ya 98, wakiendeleza ushindi wa tano mfululizo dhidi ya Barca.

Na kocha huyo raia wa Italia alisifia jitihada za wachezaji wake, ambao sasa wanatakiwa kujiandaa kwenye mchezo wa fainali utakaopigwa Jumapili.

Madrid itacheza fainali hiyo dhidi ya Atletico Madrid au Athletic Bilbao ambao walikutana jana Alhamisi kwenye nusu fainali.

"Natakiwa kuwa mkweli, Barcelona walicheza mchezo mzuri sana," alisema Ancelotti akinukuliwa na Movistar.

"Sidhani kama Barcelona walitutawala sisi, walimiliki mpira; walikuwa wazuri sana kwenye mashambulizi ya kushtukiza. Ulikuwa mchezo wa burudani sana."

# Conte ajitetea kumwacha benchi Lloris

**LONDON, England**

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte ametetea maamuzi yake baada ya kumpumzisha golikipa chaguo la kwanza, Hugo Lloris na kumwanzisha Pierluigi Gollini wakati wakifungwa na Chelsea, Jumatano.

Kipa huyo chaguo la pili, Gollini alifanya vizuri kwa kuokoa shuti la mapema la Romelu Lukaku, lakini yalikuwa ni makosa yake wakati Antonio Rudiger akifunga bao dakika ya 18.

Hilo lilikuwa bao pekee kwenye mchezo huo wa pili wa nusu fainali ya kombe la EFL na kuwafanya vijana hao wa kocha, Thomas Tuchel kutinga fainali kwa ushindi wa uwiano wa mabao 3-0. Mchezo wa kwanza waliibuka na ushindi wa mabao 2-0.


Conte alionyesha kutetea uamuzi wake wa kumuacha nahodha na golikipa huyo mzoefu Lloris, na anahisi Gollini - ambaye amecheza mechi 10 tu kwa Spurs msimu huu alistahili kuanza.

"Kabla ya hapa, Pierluigi mara zote amekuwa akicheza kwenye michuano ya Carabao na Conference Ligi," alisema Conte.

"Nafikiri unapokuwa na timu kama Tottenham, ni muhimu kutoa nafasi kwa kipa kwa sababu Pierluigi ameonyesha kuwa na uwezo.

"Halafu tunatakiwa kucheza mechi tatu ndani ya siku saba dhidi ya Arsenal, Leicester na Chelsea.

"Nafikiri anastahili nafasi hii ya kucheza kwenye mchezo muhimu. Nafikiri Gollini alicheza vizuri."



,297,200

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 15/01/22 | 18:00 | Mallorca vs Espanyol | 2.50 | 2.94 | 2.99 |
| 02. 15/01/22 | 18:15 | OH Leuven vs Mechelen | 2.31 | 3.49 | 2.81 |
| 03. 15/01/22 | 18:30 | Boavista vs Gil Vicente | 2.87 | 3.12 | 2.46 |
| 04. 15/01/22 | 20:30 | Monchengladbach vs Bayer Leverkusen | 2.54 | 3.69 | 2.49 |
| 05. 15/01/22 | 20:30 | Sporting Gijon vs Cadiz CF | 2.50 | 2.99 | 2.94 |
| 06. 15/01/22 | 20:30 | Girona vs Rayo Vallecano | 2.52 | 3.11 | 2.81 |
| 07. 15/01/22 | 20:45 | NEC Nijmegen vs Heracles Almelo | 2.35 | 3.29 | 2.85 |
| 08. 15/01/22 | 21:00 | Nancy vs Bastia | 2.70 | 3.09 | 2.60 |
| 09. 15/01/22 | 21:00 | US Quevilly Rouen vs Amiens | 2.81 | 3.20 | 2.43 |
| 10. 15/01/22 | 23:30 | Betis vs Sevilla FC | 2.57 | 3.16 | 2.71 |
| 11. 16/01/22 | 16:30 | Cambuur vs Sparta Rotterdam | 2.37 | 3.49 | 2.70 |
| 12. 16/01/22 | 17:00 | Lorient vs Angers | 2.37 | 3.19 | 3.04 |
| 13. 16/01/22 | 18:00 | Eupen vs Cercle Brugge | 2.95 | 3.35 | 2.28 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 14/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:15 | 3934 | Persik Kediri vs PS Tni | 2.80 | 3.18 | 2.33 |
| 14:00 | 4009 | FC Vizela U23 vs Vitoria Guimaraes U23 | 1.98 | 3.76 | 3.03 |
| 14:15 | 1725 | Persepam MU vs Bhayangkara Surabaya Utd | 4.83 | 3.48 | 1.65 |
| 14:15 | 4710 | Barito Putera vs Pusamania Borneo | 4.52 | 3.56 | 1.67 |
| 15:35 | 5958 | Al Raed Club vs Al Ittihad Jeddah | 3.86 | 3.81 | 1.82 |
| 15:50 | 2308 | Abha vs AL Baten | 1.93 | 3.67 | 3.57 |
| 16:00 | 1208 | Hapoel Afula vs Hapoel Ramat Gan | 2.53 | 3.18 | 2.78 |
| 16:00 | 1827 | Senegal vs Guinea | 1.73 | 3.27 | 5.35 |
| 16:00 | 4462 | Ruvu Shooting vs Mtibwa Sugar | 2.25 | 2.75 | 3.43 |
| 16:00 | 4468 | Sectzya Nes Ziona vs Hapoel Acre | 2.23 | 3.27 | 3.17 |
| 16:00 | 5578 | Hapoel Kfar Saba vs Hapoel Rishon Lezion | 2.06 | 3.37 | 3.47 |
| 16:00 | 5810 | Hapoel Raanana vs Hapoel Petah Tikva | 2.58 | 3.03 | 2.83 |
| 16:45 | 3745 | Persebaya Surabaya vs PSM Makassar | 1.50 | 3.96 | 5.60 |
| 17:00 | 2293 | RC Arbaa vs Ol. Medea | 1.78 | 3.24 | 4.35 |
| 17:00 | 5787 | FC Goa vs Northeast United FC | 1.82 | 3.66 | 3.61 |
| 17:50 | 2382 | Al-Ettifaq vs Al Shabab Riyadh | 4.95 | 4.16 | 1.59 |
| 18:00 | 1318 | Aris Limassol vs Doxa Katokopia | 1.65 | 3.72 | 5.16 |
| 19:00 | 1876 | Morocco vs Comoros | 1.22 | 5.16 | 17.85 |
| 19:00 | 2899 | MC Oran vs RC Relizane | 1.71 | 3.33 | 4.64 |
| 19:00 | 5898 | Malawi vs Zimbabwe | 3.27 | 2.92 | 2.37 |
| 20:00 | 1146 | Besiktas vs Gaziantep BB | 1.54 | 4.24 | 5.32 |
| 20:00 | 1833 | Menemen Bld vs Bandirmaspor | 3.71 | 3.42 | 1.86 |
| 20:00 | 3238 | Yeni Malatyaspor vs Goeztepe | 2.72 | 3.31 | 2.47 |
| 20:00 | 5851 | Paeek vs AEK Larnaca | 7.92 | 4.85 | 1.36 |
| 20:30 | 1738 | Hansa vs Hannover | 2.55 | 3.29 | 2.60 |
| 20:30 | 4603 | Dynamo Dresden vs Hamburger SV | 3.88 | 3.53 | 1.86 |
| 21:00 | 1811 | Creteil vs Le Mans | 2.49 | 3.08 | 2.79 |
| 21:00 | 2016 | Chateauroux vs Avranches | 1.64 | 3.71 | 4.88 |
| 21:00 | 2859 | Boulogne vs Red Star | 3.31 | 3.26 | 2.10 |
| 21:00 | 3441 | Chambly vs Saint Brieuc | 2.38 | 3.14 | 2.89 |
| 21:00 | 4334 | Sedan vs Villefranche Sur Saone | 3.82 | 3.18 | 1.97 |
| 21:00 | 4836 | TSV Havelse vs Duisburg | 4.42 | 3.68 | 1.72 |
| 21:30 | 4039 | VV Alkmaar W vs Heerenveen W | 2.39 | 3.73 | 2.42 |
| 21:30 | 4840 | Ajax W vs ADO Den Haag W | 1.29 | 6.20 | 8.40 |
| 22:00 | 2028 | NAC Breda vs FC Volendam | 3.32 | 3.67 | 1.96 |
| 22:00 | 2606 | Gabon vs Ghana | 3.97 | 3.02 | 2.05 |
| 22:00 | 2798 | Telstar vs Maastricht | 1.77 | 3.71 | 4.00 |
| 22:00 | 3287 | FC Eindhoven vs Jong Utrecht | 1.71 | 3.81 | 4.20 |
| 22:00 | 3748 | PEC Zwolle vs Willem II Tilburg | 2.08 | 3.29 | 3.39 |
| 22:00 | 4644 | VVV Venlo vs Jong PSV | 2.23 | 3.41 | 2.92 |
| 22:00 | 4670 | Emmen vs Helmond Sport | 1.31 | 5.08 | 8.01 |
| 22:00 | 5292 | Almere City vs Roda Kerkrade | 3.03 | 3.47 | 2.14 |
| 22:00 | 5583 | Dordrecht vs Jong AZ Alkmaar | 2.89 | 3.47 | 2.22 |
| 22:00 | 5843 | SBV Excelsior vs De Graafschap | 2.54 | 3.46 | 2.49 |
| 22:30 | 1161 | Borussia Dortmund vs SC Freiburg | 1.51 | 4.60 | 5.40 |
| 22:30 | 3708 | Ternana vs Ascoli | 2.08 | 3.20 | 3.50 |
| 22:45 | 3147 | Partick Thisle vs Kilmarnock | 2.44 | 3.17 | 2.78 |
| 22:45 | 5016 | KAA Gent vs Kortrijk | 1.23 | 5.70 | 11.78 |
| 23:00 | 1417 | Nice vs Nantes | 1.81 | 3.53 | 4.37 |
| 23:00 | 4173 | Brighton vs Crystal Palace | 2.07 | 3.21 | 3.76 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MABONDIA TANGA KUPAMBA USIKU WA 'BALAA JIPYA'

**Na Dennis Fussi**

MABONDIA wa Jiji la Tanga wakiongozwa na wakongwe wanatarajia kupanda ulingoni Januari 30 mwaka huu kwenye pambano la usiku wa Balaa Jipya.

Katika usiku huo, bondia Mchanja Yohana atabipagana na Mohamed Mpombo huku akisindikizwa na bondia mkongwe, Allan Kamote kwa lengo la kumpa kumsapoti.

Mchanja ambaye anashikilia mkanda wa UBO atapanda ulingoni kwenye pambano la raundi nane ambalo litapigwa kwenye Ukumbi wa Mzazi ulioko Muheza, Tanga.

Kwa mujibu wa promota wa pambano hilo, Ally Mwanzoa mabondia wakubwa wa Tanga watapanda ulingoni kusapoti pambano hilo.

"Mabondia wote maarufu wa Tanga wakiongozwa na Allan Kamote, Said Mundi, Jacob Maganga na Said Mtango watapanda ulingoni kumsapoti mwenzao asijione mpweke nyumbani kwao," alisema Mwanzoa.

Alisema Kamote na Mundi bado wapinzani wao hawajawekwa wazi, lakini Jacob Maganga atacheza na Jumanne Mohammed na Salim Mtango atapigana na Simon Zabron kwenye pambano la raundi nane.



Mkurugenzi wa Bendi ya Waluguru Original ya mjini Morogoro, Killer Boy (katikati), akifanya vitu vyake na waimbaji wa bendi hiyo, Kuruthum Abbas (kulia) na Amina Remmy, katika onyesho la bendi mjini humo hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sauti za Busara 2022 kupaza sauti za wanawake

**Na Dennis Fussi**

TAMASHA la 19 la Sauti za Busara lililoanza Januari 11, mwaka huu, Mji Mkongwe Zanzibar litafikia tamati Februari 13, huku likitambulisha muziki kutoka sehemu mbalimbali za bara la Afrika unaopigwa mubashara.

Tamasha hili linawajumuisha wanamuziki wadogo na wanaochipukia huku likitoa msisitizo kwa wanamuziki wa kike kutoka Tanzania, Uganda, Afrika Kusini, Congo na Zambia.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Tamasha hilo, Yusuf Mahmoud miongoni mwa wanamuziki watakaotumbuiza mwaka huu ni pamoja na Sampa The Great kutoka nchini Zambia ambaye huchanganyaji muziki wa mahadhi ya kufoka katika miondoko ya Kiafrika.

Mahmoud alisema wasanii wote watatumbuiza muziki wa hali ya juu wenye asili, ubunifu na wa nguvu, ambao ni Siti & The Band (Zanzibar), Msaki na Nomfusi (Afrika Kusini), Suzan Kerunen ( Uganda), Fanie Fayar (Congo) na Upendo Manase (Tanzania).

Wasanii wengine ni Sjava (Afrika Kusini), Sholo Mwamba na Bendi ya Wamwiduka (Tanzania), Maallem Abdelkebir Merchane (Morocco), Dendri Stambeli Movement (Tunisia), Sylent Nqo na Evans Mapfumo (Zimbabwe), Zan Ubuntu na Nadi Ikhwan Safaa (Zanzibar).

Kwa takriban miongo miwili, tamasha la Sauti za Busara limekuwa nguzo muhimu katika muziki wa Afrika ambalo faida zake zinakwenda mbali zaidi kwa kutoa ajira, biashara, fursa ya wasanii kujitambulisha, ushirikiano, kufahamiana, mafunzo na kukuzaji ujuzi, kuimarisha mshikamano wa kijamii, umoja na nje ya mipaka ya kikanda.

Michezo
Ijumaa Januari 14, 2022
Nipashe





## Inzaghi: Wachezaji Inter Milan watapewa zaidi

# CHAMA KUFUNGA USAJILI SIMBA SC

●●●Ni saa 24 kabla ya kufungwa kwa pazia la dirisha dogo, viongozi wameshamalizana na Berkane FC na atavaa jezi namba 17...



**Na Saada Akida, Zanzibar**

UONGOZI wa Simba umefikia hatua za mwisho katika usajili wa kiungo Clatous Chama na muda wowote nyota huyo wa nchini Zambia atatua kuungana na timu hiyo kuimarisha timu hiyo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano iliyopo mbele yao.

Hivi karibuni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez aliwaahidi mashabiki wa timu hiyo kwamba, wataletewa 'sapraizi' ambayo ni Chama, anayetarajiwa muda wowote kutua nchini.

Taarifa zilizoifikia gazeti hili jana kutoka ndani ya klabu hiyo, viongozi wa Simba tayari wameshamalizana na klabu yake ya Berkane FC na nyota huyo kwa sasa atatambulishwa rasmi kurejea kikosini.

Alisema Chama ni miongoni mwa wachezaji ambao wameongezwa katika usajili ya dirisha dogo na alitakiwa kutua nchini leo au kesho kuungana na wachezaji wenzake katika kikosi cha timu hiyo.

"Chama ndio sapraizi inayosubiriwa baada ya viongozi wa Simba kumalizana na klabu yake ya Berkane FC, muda wowote kuanzia sasa atarejea nchini na tayari ameomba kuvaa jezi yake namba 17," kwa mujibu wa taarifa hizo.

"Ombi la Chama limekubaliwa baada ya Pape Ousmane Sakho kukubali kumwachia Chama jezi namba 17 huku yeye akiomba kuvaa namba 10 iliyokuwa ikivaliwa na Ibrahim Ajibu," alisema mtoa habari huyo.

Barbara ambaye yuko visiwani Zanzibar, na alipoulizwa kuhusu nyota huyo hakutaka kuweka wazi na kudai kwamba, hivi karibuni watategua bomu katika usajili wao wa dirisha dogo unaotarajiwa kufungwa kesho Januari 15.

"Mashabiki wanatakiwa kuwa na subira kwa sababu viongozi tumekuwa makini katika usajili wetu wa dirisha dogo nani anakuja wavumilie ndani ya hizi siku mbili tutamtambulisha mchezaji ambaye tumemsajili," alisema Barbara.

## Coastal yaitishia nyau Yanga

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Coastal Union imeonya Yanga kuwa isitegemee matokeo mazuri kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga Jumapili ijayo, huku ikiikumbusha kuwa haijawahi kupata ushindi kwa misimu kadhaa.

Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Rashid Mgweno amesema kuwa wanajipanga kucheza na Yanga kama wanavyojipanga na timu nyingine, lakini wanaichukulia ni mechi kubwa na ngumu, lakini wakiwa na uhakika wa kuibuka na ushindi kutokana na historia kuibeba wanapocheza nayo kwenye uwanja huo.

Coastal Union itakuwa mwenyeji wa Yanga kwenye uwanja huo Januari 26 kwenye mechi ya raundi ya 12 ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Mechi itakuwa nzuri na ngumu. Siyo siri kuwa Yanga msimu huu ni nzuri na ina wachezaji wazuri, lakini ikumbukwe msimu uliopita tuliwafunga Mkwakwani. Kwa hiyo na sisi msimu huu tuna timu nzuri kuliko hata msimu uliopita, waje vizuri tu," alisema Mngweno.

Alisema hawataweza kukubali kufungwa kirahisi kwa sababu walipoteza mechi iliyopita nyumbani dhidi ya Mtibwa Sugar, hivyo hawawezi kuruhusu kupoteza tena.

Desemba 28, mwaka jana, Coastal ilichapwa Uwanja wa Mkwakwani bao 1-0 na Mtibwa Sugar.

Yanga haijaifunga Coastal Union kwenye Uwanja wa Mkwakwani kwa misimu saba sasa.

Mara ya mwisho Yanga kupata ushindi kwenye uwanja huo, ilikuwa ni Februari 4, 2015, Ligi Kuu msimu wa 2014/15, iliposhinda 1-0 lililofungwa na nahodha na beki wake mahiri wakati huo, Nadir Haroub 'Cannavaro' dakika ya 11 ya mchezo.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042